

**KUFANANA NA KUTAFAUTIANA KWA MAUDHUI NA FANI KATI YA  
METHALI ZAKITANZANIA NA ZA KILIBYA: UTAFITI LINGANISHI**

**HAMZA MANSOUR KHALIFA EL-JETLAWIY**

**TASNIFU YA KISWAHILI KWA MINAJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA  
YA UZAMILI (MA. KISWAHILI) KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA  
JAMII, YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2013**

**UTHIBITISHO**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii iitwayo:  
***Kufanana na Kutafautiana kwa Maudhui na Fani kati ya Methali za Kitanzania  
na za Kilibya: Utafiti Linganishi***, na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria  
cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya Uzamili katika Fasihi  
ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

-----  
Prof. Dkt. Sheikh, T.S.Y Sengo

(Msimamizi)

-----  
Tarehe

**HAKIMILIKI**

Haki ya kunakili Tasinifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, Sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali ya kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasinifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**TAMKO LA MTAHINIWA**

Mimi, **Hamza Mansour Khalifa El-Jetlawiy**, natamka na nathibitisha kwamba, Tasinifu hii iitwayo *Kufanana na Kutafautiana kwa Maudhui na Fani kati ya Methali za Kitanzania na za Kilibya: Utafiti Linganishi*, ni kazi yangu mimi mwenyewe, halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya shahada yoyote.

.....  
Hamza Mansour Khalifa El-Jetlawiy

.....  
Tarehe

**TABARUKU**

Ninatabaruku kazi hii kwa wazazi wangu nafamilia yangu na pia kwa wapenzi wote wa Fasihi hasa Methali.

## SHUKRANI

Kwanza Kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njeme na kuniweka hai mpaka leo ninapomaliza kufanya utafiti huu.

**Pili**, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Prof. Dkt. Sheikh, T.S.Y.Sengo kwa kukubali kuwa msimamizi wa kazi hii ambayokwa kawaida ingekuwa ngumu lakini kwa maarifa na ujuzi wake imefanyika kwa wepesi na mafanikio makubwa.

**Tatu**, ninapenda kumshukuru Bi Rehema A. Kassanga wa Q&S Mult-Enterprises, Mazense kwa Prof. Sengo kwa kuichapa kazi hii. Pia ninamshukuru Rafiki yangu Rajab Nassor Chande ambaye alikuwa karibu nami kila nilipomhitaji.

**Nne**, Ninapenda pia kutoa shukurani zangu nyingi kwa wazazi wangu, ndugu na familia yangu ambao wamenihimiza sana juu ya umuhimu wa wa kusoma shahada ya uzamili katika fasihi ya Kiswahili.

**Tano**, shukurani za pekee zimwendee mke wangu na watoto wangu wote kwa uvumilivu wao wakati wa masomo yangu na vile vile kwa kunitia moyo wa kusoma.

**Mwisho** lakini si kwa umuhimu ninaishukuru Serikali ya Libya kwa msaada wake mkubwa katika kufanikisha masomo yangu kukamilika tangu ngazi za awali kabisa katika elimu mpaka hii ya uzamili ninayohitimu sasa.

## IKISIRI

Utafiti huu ulihusu **Kufanana na kutofautiana kwa maudhui na fani kati ya methali za Kitanzania na Kilibya: Utafiti linganishi**. Kwa msingi huo basi, lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza kufafana na kutofautiana kwa maudhui na kwa uchache fani kati ya methali za Kiswahili na zile za Kilibya. Ili kutimiza lengo hili madhumuni mahususi yalikamilishwa. Madhumuni hayo ni Kukusanya methali za Kiswahili na Kilibya na kuzianisha katika makundi, kuchunguza kufanana na kutofautiana kidhamira na kifani kati ya methali za Kilibya na Kiswahili na kuzichambua methali zote hizi ili kupata suluhu ya tatizo la utafiti. Katika kutimiza malengo haya mbinu za ukusanyaji wa data za maktabani na maskanini zilitumika. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, methali za Kiswahili na za Kilibya zinafanana katika dhamira za elimu, malezi, maonyo, ushauri, kujali chako na udugu. Tofauti inaonekana pale ambapo methali za Kiswahili zinasisitiza zaidi juu ya umoja na udugu huku zile za Kilibya zikisisitiza zaidi juu ya kujali chako. Kwa upande wa fani tumebaini kwamba, methali za jamii hizi zinafanana katika kutoa msisitizo bayana, takriri dufu na vina. Kwa upande wa tofauti za kifani methali hizi zinatofautiana katika mtindo wa kishairi. Vile vile, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba sababu za kufanana kidhamira ni misafara ya biashara na nchi zote zipo katika bara la Afrika. Pia, sababu za kutofautiana ni tofauti za kilugha pamoja na mazingira baina ya jamii hizi mbili. Mwishoni mwa utafiti huu kumetolewa mapendekezo kwa ajili ya tafiti zijazo.

## YALIYOMO

<b>UTHIBITISHO.....</b>	<b>ii</b>
<b>HAKIMILIKI.....</b>	<b>iii</b>
<b>TAMKO LA MTAHINIWA .....</b>	<b>iv</b>
<b>TABARUKU .....</b>	<b>v</b>
<b>SHUKURANI .....</b>	<b>vi</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vii</b>
<b>MAJEDWALI .....</b>	<b>xii</b>
<b>CHATI.....</b>	<b>xiii</b>
<b>VIAMBATISHI .....</b>	<b>xiv</b>
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
<b>1.0 UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
1.1 Mada ya Utafiti .....	1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	1
1.3 Tatizo la Utafiti .....	5
1.4 Kauli ya Tatizo la Utafiti.....	5
1.5 Lengo la Utafiti .....	6
1.6 Madhumuni Mahususi.....	6
1.7 Maswali ya Utafiti.....	7
1.8 Umuhimu wa Utafiti .....	7
1.9 Vikwazo vya Utafiti .....	8
1.9.1 Utatuzi wa Vikwazo.....	8
1.10 Mipaka ya Utafiti .....	8



1.11 Hitimisho.....	9
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>10</b>
<b>2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .....</b>	<b>10</b>
2.1 Utangulizi.....	10
2.2 Asili ya Lugha ya Kiswahili.....	10
2.3 Sababu ya Kuteuliwa Lahaja ya Kiunguja.....	18
2.4 Lahaja ya Kilibya .....	18
2.4.1 Asili na Sifa za Lahaja ya Kilibya.....	19
2.5 Maana ya Methali.....	20
2.6 Fani katika Methali .....	26
2.7 Hitimisho.....	35
<b>SURA YA TATU .....</b>	<b>36</b>
<b>3.0 NADHARIA ZA UHAKIKI WA FASIHI .....</b>	<b>36</b>
3.1 Utangulizi.....	36
3.2 Nadharia ya Simiotiki .....	36
3.3 Nadharia ya Umarx .....	38
3.4 Nadharia ya Dhima na Kazi .....	39
3.5 Nadharia ya Uamilifu.....	39
3.6 Nadharia ya Umuundo .....	40
3.7 Hitimishi.....	40
<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>41</b>
<b>4.0 MBINU ZA UTAFITI.....</b>	<b>41</b>
4.1 Utangulizi.....	41
4.2 Usanifu wa Utafiti .....	41

4.3 Ukusanyaji wa Data .....	42
4.3.1 Data za Upili .....	42
4.3.2 Data za Msingi .....	42
4.3.2.1 Usaili .....	43
4.3.2.2 Hojaji.....	43
4.3.2.3 Ushuhudiaji .....	44
4.4 Sampuli na Usampulishaji .....	44
4.4.1 Sampuli Nasibu .....	45
4.4.2 Sampuli Lengwa.....	45
4.5 Vifaa na Zana za Utafiti .....	46
4.6 Matatizo katika Ukusanyaji wa Data .....	47
4.7 Data Zilizokusanywa.....	48
4.8 Hitimishi.....	48
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>49</b>
<b>5.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI</b> <b>.....</b>	<b>49</b>
5.1 Utangulizi.....	49
5.2 Uchambuzi wa Data .....	49
5.3 Kuainisha Methali Zinazofanana .....	49
5.3.1 Elimu .....	50
5.4 Udugu.....	56
5.5 Malezi.....	59
5.6 Kuthamini Kilicho Chako .....	62
5.7 Tahadhari (Maonyo na Masuto).....	66

5.8 Mfanano Uliopo kati ya Methali za Kilibya na Kitanzania Kimaudhui na fani .	69
5.10 Sababu za Kufanana na Kutafautiana kwa methali za Kilibya na Kiswahili .....	78
5.10.1 Sababu za Kufanana Kifani.....	78
5.10.2 Sababu za Kutafautiana Kifani.....	78
5.11 Hitimishi.....	79
<b>SURA YA SITA.....</b>	<b>80</b>
<b>6.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>80</b>
6.1 Utangulizi.....	80
6.2 Muhtasari na Hitimishi.....	80
6.3 Hitimishi.....	82
6.4 Mapendekezo .....	83
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>85</b>
<b>VIAMBATISHO .....</b>	<b>89</b>

## **MAJEDWALI**

Jedwali Namba 1: Maeneo mnamotumika Lahaja ya Kilibya .....	19
Jedwali Namba 2: Sampuli ya Watafitiwa na Idadi yao .....	45
Jedwali Namba 3: Wazungumzaji wa Kiswahili na Kilibya.....	46

## **CHATI**

Kielezo Namba 1: Kuenea kwa Kiswahili .....	16
Kielezo Namba 2: Nadharia ya Uhamishaji Maana.....	31

## **VIAMBATISHI**

Kiambatisho Namba 1: Dodoso kwa Ajili ya Usaili, Walengwa ni Wazeee .....	89
Kiambatisho Namba 2: Hojaji, Walengwa ni Vijana.....	90

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### 1.1 Mada ya Utafiti

Kwanza kabisa, napenda kutanguliza kusema kwamba utafiti huu unahusu *Kufanana na Kutafautiana Kwa Maudhui na Fani kati ya Methali za Kitanzania na za Kilibya - Utafiti Linganishi*. Vile vile, utafiti huu utafanyika katika vitongoji kadhaa vya Libya, sambamba na vya nchini Tanzania katika maeneo ambayo yana wazungumzaji wengi wa lugha ya Kiswahili kama ilivyoainishwa katika sura ya nne ya utafiti huu. Hivyo basi, itakuwa rahisi kupata data kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili ambao wao ndio tegemeo kubwa la utafiti huu, kwani kwa kupitia ndimi na majawabu yao ndio ukamilifu wa utafiti huu unakuwa umekaribia au umefikia lengo lililokusudiwa.

#### 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Katika ubunifu wa kazi za fasihi, wasanii hutumia lugha ya kawaida na lugha ya kitamathali kuwasilisha ujumbe walioukusudia kutegemeana na maudhui, muktadha na wakati maalum (Njogu na Chimera, 1999). Hivyo basi, katika fasihi simulizi lugha ina umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maana na ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa. Senkoro (2011) kwa upande wake anasisitiza kwamba, kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila kuwa na maarifa ya lugha ambayo ndiyo njia ya kujieleza. Kwa hiyo, ni lazima kuchunguza vipengele vya lugha fulani jinsi na namna msanii anavyovitumia kwa kuvihusisha na malighafi za lughawiya ili kuelewa kile kinachowasilishwa na msanii fulani katika kazi yake. Lugha katika fasihi ni tasinia pana isiyoweza kuelezeka kwa mara moja na

ikakamilika kwa kuwa ina vipengele vingi. Kwa mfano lugha hujumuisha tamathali za usemi ambazo kwa hakika ni nyingi sana. Katika utafiti wetu huu tumechunguza kipengele kimoja tu cha tamathali za usemi ambacho ni methali. Wataalamu wa kazi za fasihi kama vile Senkoro (1982) anaeleza kwamba, methali ni aina ya tamathali ya usemi iliyo na historia ndefu katika maendeleo ya fasihi simulizi. Anaendelea kueleza kwamba, aina hii ya tamathali imetoa mchango muhimu katika kuadilisha jamii si tu ya Kitanzania, Afrika bali duniani kote.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba, methali ni tamathali ya usemi iliyotumika katika kufundisha na kujinzia maarifa mbalimbali kabla ya ujio wa elimu iliyotolea na Wakoloni na Waarabu kwa upande wa Afrika na jamii mbalimbali duniani. Njogu na Chimerah (1999) kwa upande wao wanaeleza kwamba, methali ni tamathali ambayo bado ina umuhimu mkubwa katika kufunza maadili mbalimbali katika jamii na kwamba ndo maana methali zinaendelea kufundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini hasa katika taaluma ya fasihi. Kutokana na kufundishwa methali katika ngazi mbalimbali za elimu, wanafunzi hupata maarifa juu ya mambo mbalimbali kama vile historia ya jamii yao, asili yao, mila na desturi zao pamoja na kanuni na taratibu za maisha katika jamii husika.

Senkoro (2006) kwa upande wake anasema kwamba, kutokana na umuhimu wa methali katika jamii imewafanya watafiti mbalimbali kufanya tafiti zao katika kuibua masuala mbalimbali yanayopatikana katika methali hizo. Miongoni wa watafiti hao ni Finnegan (1970) na Okphweho (1992) ambao wamechunguza fasihi simulizi kwa ujumla methali zikiwemo. Katika maelezo yao tunapata uelewa kwamba, methali ni



tamathali muhimu katika fasihi ya Mwafrika na kupitia methali hizo ndimo falsafa juu ya maisha ya jamii za Kiafrika huibuliwa na kuhifadhiwa. Watafiti hawa wanaendelea kueleza kwamba, methali huwasilishwa kwa kutumia lugha za aina mbalimbali na kwa kiasi kikubwa ikiwa ni ile ya mafumbo iliyojaa taswira, picha, sitiari na ishara.

Mturo (2011) alifanya utafiti wa kuchunguza semi mbalimbali zinazoandikwa katika daladala zinazopatikana Dar es Salaam ili kubainisha ufasihi unaopatikana katika semi hizo. Pamoja na mambo mengine utafiti wake ulibaini kwamba, mojawapo ya semi zinazopatikana katika daladala hizo ni methali. Hii inaonesha kwamba, methali ni tamathali ya usemi inayokubalika kwa kiasi kikubwa katika jamii. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mahenge (2009) ambaye alichunguza ufasihi wa semi ziandikwazo katika tiketi za daladala jijini Dar es Salaam. Kutokana na maelezo haya tunapata kutambua kwamba methali ni aina ya tamathali ya usemi iliyo na umuhimu mkubwa katika kutoa maadili, maonyo, kukumbusha mema na kukataza mabaya na kadhalika katika jamii.

Hivyo basi, umuhimu wa methali katika jamii haupo katika jamii ya Kitanzania peke yake bali katika jamii nyingi duniani jambo ambalo linatufanya tufanye utafiti linganishi kuhusu methali. Utafiti huu linganishi unahusu methali za Kitanzania na zile za Kilibya. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu umechunguza methali katika jamii mbili zenye utamaduni tafauti, lugha na maeneo ya kijiografia tafauti, ni jamii zenye tafauti pia za kiuchumi, kisiasa na kijamii ili kuona ni jinsi gani methali hufanana na kutafautiana katika muundo na matumizi ya muktadha huo tofauti.

Methali ni semi fupi zenye kutoa ujumbe mzito na kwa haraka (Wamitila, 2008). Methali huwa zimejaa hekima ndani yake. Semi hizi hutumia lugha ya mkato yenye mapigo maalumu ambayo huleta ladha ya kishairi (Njogu na Chimera, 2009). Methali hutumia tamathali mbalimbali kama chuku, sitiari, n.k. Vilevile, methali hutumia lugha ya picha; kwa mfano:

Yaliyompata pekunaungo yatampata

Peku ni ungo uliotumiwa kwa muda mrefu na kuchakaa kiasi kwamba unavujisha kile kinachopetwa. Na ungo ni aina ya chombo ambacho Waswahili hutumia kuchungia (kupepetea) mchele, mbaazi mahindi na kadhalika.

**Maana:** - Ni kwamba usimdharau mtu aliyefikwa na baya lolote au aliyekuwa katika hali mbaya kwani hayo ni mapito ya maisha tu, yeye katangulia na wewe litakukuta tatzizo lako.

**Kwa Kilibya:-** اللي اتعشخو كاتغداك

**Kwa Kilatini :** Ellee taa shaa khuuk et ghaddaak

**Tarjama yake:** Aliyemfanyia uadui nduguyo atamalizia **kwako** (linganisha) mfanano wa kitaswira kati ya peku na nduguyo, na kati ya ungo na kwako wewe mwenyewe, utaona kwamba kusudio la kutochekana katika mabalaa linakusanyika moja kwa moja katika methali ya Kilibya na ya Kiswahili ijapokuwa kila moja imetumia tasira yake.

Mfano wa methali hapo juu unaonesha kwamba, katika jamii ya Kilibya nayo kuna matumizi ya methali katika mawasiliano yao. Kwa hivyo basi ni imekuwa ni rahisi kwetu kufanya utafiti linganishi kati ya methali za Kilibya na za Kitanzania katika dhamira na baadhi ya vipengele vya fani ili kuona ufanano na utofauti wake.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Methali ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa katika kazi za fasihi ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa. Tamathali za usemi kama kipengele cha lugha hujitokeza katika kazi za fasihi kulingana na wakati, muktadha na matumizi ya jamii moja na nyingine. Kila jamii inayohusika huibua methali zake kulingana na muktadha wake ili kufikisha ujumbe kwa jamii yake. Watafiti kadhaa tuliowanisha katika usuli hapo juu wanaonesha kwamba, methali ni aina ya tamathali ya usemi iliyo na umuhimu mkubwa katika jamii kwa kuwa ni chombo cha kufunza maadili, kuonya na kueleza falsafa nzima ya maisha ya jamii husika. Pamoja na kuwepo umuhimu huu wa methali hakuna utafiti wa kina uliokwishaanyika kwa malengo ya kulinganisha methali za mataifa tofauti ili kubainisha ni namna gani zinafanana ama kutofautiana katika kutoa maadili, kuonya na kueleza falsafa nzima ya maisha ya jamii zake. Utafiti huu umefanywa ili kuziba pengo la kiutafiti katika kufananisha na kutofautisha methali za jamii ya Waswahili na zile za Walibya.

### **1.4 Kauli ya Tatizo la Utafiti**

Utafiti huu unachunguza fasihi simulizi, kipengele cha methali. Jamii nyingi za Kiafrika zimeanza kusahau mila na desturi za mababu zao ambao walikuwa wakiwapa mafunzo kwa kutumia methali. Watoto wengi wa kizazi cha leo mara nyingi wamekuwa hawashiriki katika shughuli za kimila kutokana na muda mwingi kuwa mijini. Vijijini hufika endapo tu kumetokea msiba, harusi au kwa shughuli maalumu. Ile jadi ya kukaa na wazee na kutaniana nao kwa mambo tofauti, kushauriana na kuwauliza kuhusu changamoto za kimaisha, kukusanyika kwa watoto kwa pamoja na kutamba hadithi mbalimbali, ambazo miongoni mwa hizo huwa kuna

methali zinazokusudia kufikisha ujumbe fulani, kupeana vitendawili na mengineyo yasiyokuwa hayo, yote haya yameanza kupotea kwa kiasi kikubwa sana. Kusahaulika kwa mila na desturi hizo kumetokana na kuingia kwa utandawazi ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa mila na desturi za jamii mbalimbali za Kiafrika hasa kwa kuiga mambo mengi ya kigeni. Ni kweli katika juhudi za kuhakikisha kuwa jadi zetu hazipotei, kuna baadhi ya idhaa za televisheni zinajitahidi kuweka vipindi vya hadithi za watoto na vitendawili, lakini hili bado halijaweza kufanya kazi ile ya zamani iliyorithisha vizazi kwa vzazi methali na hekima za Mwafrika.

Kutokana na mambo hayo, utafiti huu wa kufanana na kutafautiana kimaudhui na fani kwa methali za jamii ya Walibya na ya Watanzania una madhumuni ya kukumbushia na kufufua methali za jamii hizo ambazo zalikuwepo hapo kale, ili kurudisha dhima zake katika jamii kufanya hivyo ni kwa lengo la kuhifadhi tamaduni yetu ya Afrika.

### **1.5 Lengo la Utafiti**

Utafiti huu unalenga kuchunguza kufanana na kutafautiana kwa kwa maudhui na kwa uchache fani kati ya methali za jamii ya Watanzania wanaozungumza lugha ya Kiswahili na methali za jamii ya Walibya watumiao lugha ya Kilibya katika muundo na matumizi.

### **1.6 Madhumuni Mahususi**

- 1 Kukusanya methali katika lugha za Kilibya na Kiswahili na kuziainisha katika makundi.

- 2 Kuchunguza kufanana na kutafautana kifani na kidhamira kwa methali za Kiswahili na za Kilibya
- 3 Kuzichambua methali zote hizo ili kupata suluhu ya tatizo la utafiti.

### 1.7 Maswali ya Utafiti

- 1 Ni zipi methali za Kiswahili na zile za Kilibya?
- 2 Kuna ufanano na utafauti gani kati ya methali za Kiswahili na zile za Kilibya?
- 3 Methali hizi zinasaidiaje kuleta suluhu ya tatizo la utafiti?

### 1.8 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaumuhimu mkubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya taaluma ya fasihi na Kiswahili kwa ujumla. Umuhimu huo unaonekana katika maeneo yafuatayo:

**Kitaaluma:** Utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu katika tasnia ya fasihi ya Kiswahili hasa fasihi simulizi hususani kipengele cha methali. Wanafunzi wanaosoma katika shahada za awali mpaka ile ya uzamivu watauona utafiti huu kama kichocheo katika tafiti zao. Wanataalimu wa fasihi nao watautumia utafiti huu katika marejeleo yao kama sehemu ya kukamilisha tafiti zao.

**Kinadharia:** Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa katika kuthibitisha nadharia za Kifasihi kwamba kila jamii ina utamaduni na fasihi yake. Hili linaonekana pale ambapo tumbaine kwamba, Walibya kama ilivyo kwa Waswahili nao wana methali zao ambazo zinafanana na kutofautiana.

**Kimahusiano:** Utafiti huu ni muhimu kwa sababu unaendelea kukuza mahusiano mazuri baina ya nchi za Libya na Tanzania. Inakuza mahusiano kwa sababu kuainisha methali kama tulivyofanya kunatufanywa tuelewe vizuri tamaduni zilizopo

baina ya mataifa haya mawili na hivyo kuwafanywa wananchi wa pande zote kufahamu utamaduni wa mwenzake na kisha kutembeleana kwa namna mbalimbali.

**Kiualimu:** Utafiti huu ni sehemu muhimu katika kufunza mema na kukataza mabaya katika jamii za pande zote mbili kutokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya maudhui yapatikanayo katika methali huwa yanatoa mafunzo yenye maadili kwa jamii husika. Hivyo basi, utafiti huu ni mwalimu tosha wa maadili katika jamii.

### **1.9 Vikwazo vya Utafiti**

Kikwazo kikubwa katika utafiti huu ni suala ya lugha mama ya mtafiti. Mtafiti ni mzaliwa wa Libya na lugha mama yake ni Kiarabu hivyo Kiswahili hakielewi vizuri kama vile anavyokielewa Kiarabu. Kwa hali hii ilikuwa vigumu kwake kuelewa baadhi ya misamiati inayopatikana katika methali za Kiswahili kwa ufasaha wake.

#### **1.9.1 Utatuzi wa Vikwazo**

Mtafiti alilazimika kutafuta msaidizi ambaye ni Mswahili ambaye alimsaidia katika kufafanua dhana mbalimbali ambazo zilikuwa ngumu kueleweka katika methali za Kiswahili. Ufafanuzi huo ulimsaidia mtafiti katika kukamilisha malengo ya utafiti wake.

### **1.10 Mipaka ya Utafiti**

Pamoja na kuwepo kwa wazungumzaji wengi wa Kiswahili nchini kote Tanzania. Utafiti huu utahusisha wazungumzaji wa Kiswahili kutoka katika baadhi ya mikoa ya Tanzania. Lakini wazungumzaji wa Kiswahili wa mkoa wa Dar es salaam watakuwa na nafasi kubwa kuliko wa mikoa mingine. Mkoa huu umeteuliwa kwa kuzingatia kuwapo kwa takriban makabila yote ya Tanzania yazungumzayo Kiswahili.

Ni ukweli usiopingika kwamba jiji la Dar es salaam limepoteza sifa yake ya upwani kwa maana ya utamaduni, kwa vile linakaliwa na watu wa makabila mchanganyiko ya Tanzania na ya nje ya Tanzania. Uswahili waMrima (KI-<sup>1</sup>MRIMA-) na Wa shomvi (KISHOMVI<sup>2</sup>: kunduchi ya kale) haupo tena. Mchanganyiko huu wa makabila tafauti ya Kitanzania licha ya kupoteza sifa ya upwani wa jiji la Dar es salaam lakini pia unaakisi matumizi halisi ya kiswahili fasaha kwa makabila hayo, hili linaweza kumfanya mtafiti aseme kuwa: **Jiji la Dar es salaam ndiyo mji mkuu wa wa lugha ya Kiswahili hivi sasa.** Profesa Sengo (2009) anasema (Fasihi ina kwao). Methali kwa lugha ya Kiswahili ni zile za makabila yote mengine, nje ya Uswahilini, zitachanganywa na za Waswahili wenyewe kwa kufananishwa na kutafautishwa na zile za Kilibya.

### 1.11 Hitimishi

Katika sura hii tumetoa utangulizi wa vipengele mbalimbali ambavyo ndivyo vitoavyo dira na mwelekeo wa utafiti wetu. Miongoni mwa vipengele hivyo ni pamoja na mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, kauli ya tatizo, malengo ya utafiti; madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti na mwisho ni mipaka ya utafiti.

---

<sup>1</sup> Kimrima ni ile tamaduni na lugha inayozungumzwa sehemu za mwambao kuanzia Vanga, Tanga, Pangani, Dar es Salaam, Rufiji na Mafia.

<sup>2</sup> Kishomvi ni tamaduni na lugha iliyotumika kwa watu wa Bagamoyo Mzizima, Dar es Salaam ya sasa hadi Kilwa.

## **SURA YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii inafanya mapitio ya kazi Tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti ili kuona wanataalimu wengine wanazungumza nini kuhusiana na mada ya utafiti wetu. Ili kupata mwelekeo wa utafiti wetu tumelazimika kupitia machapisho yanayozungumza juu ya asili ya chimbuko la lugha ya Kiswahili. Tumeamua kufanya hivi ili kujenga hoja kwamba methali za Kiswahili si za Kiarabu kama ilivyokuwa imeelezwa hapo awali kwamba Kiswahili ni Kiarabu jambo ambalo si kweli. Maelezo juu ya hili ni kama ifuatavyo:

#### **2.2 Asili ya Lugha ya Kiswahili**

Kuna tafauti kati ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili kuhusiana na uasili wake, wako wanaosema kuwa Kiswahili asili yake ni Kiarabu kwa hoja kwamba:-

- (i) Maneno yenye asili ya Kiarabu yaliyomo katika Kiswahili ni ishara tosha kwamba, lugha hii ilianza pijini ya Kiarabu.
- (ii) Neno lenyewe Kiswahili ambalo asili yake ni Kiarabu.
- (iii) Inadaiwa kwamba, Kiswahili kilianza pwani kwa kuwa idadi kubwa ya wenyeji wa pwani ni waislamu, na kwa kuwa Uislam uliletwa na Waarabu, basi Kiswahili nacho kililetwa na Waarabu.

Masebo na na Nyangwine (2009) katika kuzidhoofisha hoja hizi wanasema kwamba, madai yao hayana mashiko, lugha ya Kiswahili imetokea kuwa na maneno ya mkopo



yenye asili ya Kiarabu, na kwa hakika yapo yenye asili ya Kiajemi, Kireno, Kihindi, Kijerumani, Kiingereza n.k. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kulikuwa na mawasiliano ya karne na karne baina ya wenyeji wa pwani na wafanya biashara wa Kiarabu. Wasemaji wa lugha mbili tofauti wanapokutana hawaachi kuathiriana kilugha. Kwa hiyo kuwa na maneno mengi ya mkopo kutoka lugha nyingine hakuifanyi lugha hiyo isemekane kuwa imetokana na lugha hiyo nyingine.

Kigezo cha dini nacho hakikubaliki, lugha haiwi lugha kwa sababu ya imani, hata hivyo lugha ya Kiarabu yenyewe ilikuwepo karne nyingi kabla ya majilio ya Uislam, kama ambavyo lugha nyingine za Kimagharibi zilivyokuwepo karne nyingi za kabla majilio ya Ukristo. Kiingereza au Kijerumani si Ukristo wala Kiarabu si Uislam ila tunaweza kutumia lugha kufasili dini, lakini hatuwezi kutumia dini kufasili lugha.

Dhana ya kwamba Kiswahili asili yake ni ya Kiarabu eti kwa hoja kwamba neno lenyewe tu peke yake “Sahili” linaelekeza usuli wa lugha hiyo, au kwa kuwa lugha ya Kiswahili ina maneno mengi ya Kiarabu, hii haikubaliki, kwa sababu kabla ya kuja Waarabu Waswahili walishakuwa na lugha yao wao wenyewe inaowaunganisha, Ujaji wa Waarabu uliongezea tu baadhi ya maneno, ni sawa na ujaji wa wageni wengine ambao lugha za ziliongezea lugha ya Kiswahili baadhi ya maneno.

Ikumbukwe kwamba Wakoloni walipoivamia Afrika kwa lengo la Kuteka mali zilizomo katika bara hilo, walitumia sera na visingizio tafauti, walidai kwamba Afrika ni bara lenye kiza na watu wake ni wajinga sana, hivyo ni lazima

Wastaarabishwe. Cha kushangaza Waafrika hao hao ambao hawana ustaarabu, ndio wanaowasoma huko Ulaya katika vyuo na taasisi zao maalumu kuhusiana na Afrika. Sasa swali la kujiuliza ni kwamba, kwa nini wapoteze muda, hali na mali zao kwa ajili ya watu wajinga? Na kabla ya hapo walishazusha nadharia ijulikanayo kama “Semitiki” ambayo inawagawa watu dunia nzima katika matabaka matatu, na tabaka la mwisho katika hao ni Waafrika, ambao wamo kati yao wenye lugha za Kisemitiki. Lengo la nadharia hii ni kuwadunisha Waafrika kwanza, na kuwanyanyua Wazungu, kama ambavyo linataka kuzifanya lugha kadhaa duniani kuwa hazina asili, Kiswahili kikiwemo.

Zikaifanya lugha ya Kiswahili na lugha kadhaa asili yake ni Kiarabu. Huu ni mtazamo wa kibinafsi hauna nia nzuri na asili ya Mwafrika. Waafrika hawakuwa wajinga, walikuwa na tamaduni na ustaarabu wao wa Kiafrika kama ambavyo mabara mengina yana ustaarabu na tamaduni zao. Waarika walikuwa na lugha zao kama wengine. Na lugha ni kiashiria tu au kiunganishi kati ya watu ili wafahamiane, na lugha zote zimeumbwa na Mungu kwa lengo hilo, hakuna lugha iliyo bora kuliko nyingine. Na hakuna lugha iliyokamilika, na ndio maana Wazungu kwa kuwa hawana kiashiria kinachotaja chakula “Ugali” wanalazimika kutumia neno hilo hilo, na huku ni kutumia lugha ya mwingine, na siyo kuazima.

Hivyo si sahihi kudai kwamba lugha fulani imeazima neno kutoka kwa lugha nyingine, kwani uazimaji wa kitu maana yake ni kukirudisha baadaye, na kama hakikurudishwa kikawa kimechukuliwa moja kwa moja basi kimeibwa, na haijawahi kusikika kwamba kuna lugha iliazima neno la lugha nyingine kisha ikalirudisha. Hii ni kumaanisha kwamba lugha hiyo inatumia neno la lugha nyingine kwa sababu

haina kiashiria cha neno hilo, na utumiaji wa maneno ya lugha nyingine umo katika takriban lugha zote, si Kiswahili tu peke yake.

Maganga (1997) anaeleza kuwa Historia ya Kiswahili imeanza takriban miaka 1000 iliyopita kwenye pwani ya Afrika ya Mashariki. Inaendelea kueleza kuwa: Neno **Swahili** ni neno la asili ya Kiarabu **Sahil** lenye maana ya pwani; sawahil ’’as-sawāhilī’’ (السواحلي) ni wingi wake kwa kumaanisha yote yanayohusiana na pwani, watu au utamaduni wa eneo la pwani.

Na kuna wataalamu wengine wanaona kuwa lugha ya Kiswahili asili yake ni Kibantu. Na nadharia hii ndiyo anayoiunga mkono mtafiti. Wikipedia ikifafanua zaidi kuhusu historia ya lugha ya Kiswahili inasema (Kiswahili kilianza kama lugha ya miji na mabandari ya biashara ya kimataifa kwenye pwani la Afrika ya mashariki. Tuna historia jinsi gani miji kama vile Kilwa, Lamu na mingine kadhaa ilianzishwa na wafanyabiashara Waarabu au Waajemi waliooa wenyeji. Idadi ya wahamiaji kutoka Uarabuni haikuwa kubwa sana, hivyo lugha ya wenyeji ilitumika kila mahali ila tu maneno mengi yameingia kutoka Kiarabu. Kwa ujumla Kiswahili kina maneno ya asili ya Kiarabu kati ya 30-40%, hali inayolingana na kiasi cha maneno ya asili ya Kilatini au Kifaransa katika lugha ya Kiingereza. Hivyo Kiswahili kilizaliwa kuwa lugha ya Kibantu kilichopokea maneno mengi ya asili ya nje.

Katika kusesitiza kuwa Kiswahili sili yake ni Kibantu, Masebo na Nyangwine (2009) anasema kuwa, Meinhof na Rohl wao wanaamini kuwa, wakati wa utawala wa Washirazi katika upwa wa Afrika ya Mashariki kulikuwa na kabila la Waswahili ambalo ni dhuria la Wazaramo wa leo. Kwa sababu wao walikuwa wamezaliwa

katika harakati za kibiashara, hivyo, wakafuata nyayo za wazazi wao. Lugha yao ilikuwa ya Kibantu, na kwa kuwa Wabantu ni wengi zaidi lugha yao ikaanza kutumika na kuenea katika makabila mengine. Baadaye kwa sababu Waswahili walifanya biashara na Waarabu, Washirazi, Wamalaysia, Wahindi na Wareno, vifaa vya majina ya vitu vya biashara vya wageni vikaselelea na kuingizwa katika mfumo wa lugha hiyo ya Kibantu. Hii ndiyo nadharia ianyoelekea kukubalika kuwa ndiyo sahihi juu ya asili ya Kiswahili. Na hata historia inathibisha kuwa lugha ya Kiswahili ilizungumzwa katika upwa wa Afrika ya Mashariki hata kabla ya ujio wa wageni kama vile Waarabu na Wazungu. Ushahidi huu ulitolewa na wageni mbalimbali waliofika hapa Afrika mashariki kama vile Bin Batuta, Marco Polo na wengineo).

Kihore (1984) aneleza kwamba, Lugha ya kiswahili imeandikwa kwa herufi za Kiarabu tangu karne ya 13 BK. Kwa bahati mbaya hatuna maandiko ya kale sana kutokana na hali ya hewa kwenye pwani isiyosaidia kutunza karatasi za kurasa, kwa kuwa karatasi zenyewe zinaweza kuoza kutokana na unyevu hewani pamoja na wadudu wengi walioko katika mazingira ya pwani. Lakini maandiko ya kale yanayopatikana kutoka karne ya 17 BK huonyesha ya kwamba tenzi na shairi zinafuata muundo inayotangulia maandiko yenyewe kwa karne kadhaa. Sehemu kubwa ya maandiko ya kale ni tenzi yaani mashairi yenye aya maelfu. Tenzi ndefu kabisa inahusu kifo cha Mtume Muhamad ikiwa na aya 45,000).

Kiswahili kimepokelewa kirahisi na wenyeji kwa sababu wenyeji walikosa lugha ya pamoja kati yao, lugha za Kibantu ziko karibu sana na athira ya Kiarabu ilikuwa imeenea kote pwani. Haya yote yalisaidia kujenga umoja wa Kiswahili katika eneo kubwa la pwani la Afrika ya Mashariki.

Kufika kwa Wareno Afrika ya Mashariki kuanzia mwaka 1500 kulileta athira mpya ikiwa maneno kadhaa ya Kireno yameingia katika Kiswahili kama vile "bendera" na "meza". Kuwepo kwa wafanyabiashara Wahindi katika miji mikubwa ya pwani kuliingiza pia maneno ya asili ya Kihindi katika lugha kama vile "lakhi", "gunia" n.k. Athira ya lugha za Kihindi iliongezeka kiasi baada ya Waingereza kuwatumia Wahindi wengi kujenga reli ya Uganda.

Kiswahili kilitumika katika kanda ndefu sana kutoka Somalia hadi Msumbiji mwa Kaskazini. Wafanyabiashara Waswahili waliendeleza biashara ya misafara hadi Kongo. Kiswahili kiliendelea kuenea kwenye njia za misafara hii. Kila msafara ulihitaji watu mamia hadi maelfu wa kubeba mizigo ya biashara kutoka pwani hadi pale msafara ulipolenga hata Ziwa Tanganyika. Watu hawa wote walisambaza matumizi ya Kiswahili katika sehemu za ndani. Lakini katika maeneo fulani biashara hii ilijenga pia kizuizi. Watu kama Waganda waliona Kiswahili ni lugha ya Waislamu tena lugha ya biashara ya watumwa hadi leo ni wagumu kukubali Kiswahili. Kiswahili kilitumika kama lugha ya biashara baina ya watu wa pwani na bara. Ramani inayofuata inaonyesha sehemu zilizoenea lugha ya Kiswahili.

Ni wazi kwamba hapo zamani lugha ya Kiswahili iliandikwa kwa herufi za Kiarabu, jambo ambalo kwa upande mmoja linazidi kuweka wazi ni jinsi gani kuna uwiano na muingiliano wa kitamaduni kati ya jamii ya Waafrika inayokusanya Waarabu na Wasiokuwa Waarabu. Dhana iliyojaa kwa Waganda wengi kwamba Kiswahili ni lugha ya watumwa kwa hoja kwamba wale makuri waliokuwa wakibebeshwa mizigo walikuwa ni waswahili, ni dhana potofu ambayo msingi wake ni dhaifu au haina

mashiko kabisa, kwani hata katika jamii ya Waganda wapo makuri waliobebeshwa mizigo kama Waswahili, lakini hili halikuwafanya wale wasiokuwa waganda waizingatie lugha hiyo ya kiganda (Buganda) kuwa ni lugha ya utumwa.



**Kielezo Namba 1: Kuenea kwa Kiswahili**  
Chanzo: Mtafiti, 2013

#### Ufunguo

- Sehemu inayozungumzwa sana Kiswahili
- Sehemu inayozungumzwa Kiswahili kwa uchache mno
- Bahari na Maziwa

Kwa upande mwingine lugha ya Kiswahili kuandikwa kwa herufi za Kiarabu ni kumaanisha moja ya mambo mawili kwamba Waswahili, ima hawakuwa na herufi zao wenyewe zinazojitegemea kama vile Wachina au Wahindi na wengineo, au walikuwa na herufi zao isipokuwa kwa kuwa matamshi ya Kibantu ambayo yalikuwa na athari za Kiarabu yaliweza kuzitaifisha herufi za Kiswahili hatimaye herufi za Kiarabu kushika hatamu ya kutumika kimaandishi katika lugha ya Kiswahili, hii ni

pamoja na kukumbuka kwamba asilimia 30 au 40 za maneno ya Kiarabu zilikuwa ni kama chachu ya kukamata nafasi ya herufi hizo. Miongoni mwa ushahidi kwamba Waswahili walitumia herufi za Kiarabu, ni kwamba mpaka sasa bado kuna sehemu kadhaa ndani ya Tanzania ili barua ya posa iwe ni ya kuheshimika basi inatakiwa iwe imeandikwa kwa herufi za Kiarabu.

Kwa kuwa herufi za Kiarabu zilikuwa ndizo zikitumika katika ngazi tofauti za serikali bali hata za kijamii katika miamala mbalimbali, swali ambalo linahitaji jawabu ni kwamba muda gani herufi za Kilatini zilianza kushika hatamu ya matumizi katika sekta tofauti hatimaye katika miamala ya kijamii kwa jumla? Katika kujibu swali hili Wikipedia inaeleza: (Karne ya 19 BK ilileta utawala wa kikoloni. Wakoloni walitangulia kufika katika mabandari ya pwani wakatumia mara nyingi makarani, askari na watumishi kutoka eneo la pwani wakijenga vituo vyao barani. Watu hawa walipeleka Kiswahili katika pembe za bara.

Wajerumani waliamua kutumia Kiswahili kama lugha ya utawala katika Afrika ya Mashariki ya Kijerumani. Hapo waliweza kutumia kazi ya Wamisionari wakristo wa awali hasa Ludwig Krapf waliowahi kufanya utafiti wa lugha na kutunga kamusi na sarufi za kwanza pamoja na kuunda mfumo wa kuandika Kiswahili kwa herufi za Kilatini. Waingereza baada ya kuchukua Tanganyika kutoka kwa Wajerumani waliendela kutumia Kiswahili kama lugha ya utawala. Kuanzia mwaka 1930 waliunda kamati yenye shabaha ya kuunganisha lahaja mbalimbali na kuunda Kiswahili cha pamoja kwa ajili ya Afrika ya Mashariki (Inter-territorial Language (Swahili) committee for the East African Dependencies). Mwenyekiti wake alikuwa Frederick Johnson, makatibu R.K. Watts, P.Mzaba na Seyyid Majid Khalid

Barghash. Kamati hii iliamua kutumia lahaja ya Kiunguja kuwa msingi wa Kiswahili cha pamoja kilichoendela kufundishwa mashuleni. Leo hii ni Kiswahili rasmi kinachofunzwa kwa wanafunzi na kuandikwa magazetini na vitabuni).

### **2.3 Sababu ya Kuteuliwa Lahaja ya Kiunguja**

Wenda ikawa sababu kubwa ya kuteuliwa lahaja ya Kiunguja kuwa ndio msingi wa Kiswahili sanifu ni kwamba, lahaja hii ilikuwa imeenea sehemu kubwa sana na kueleweka katika nchi zilizokusudiwa; Zanzibar, Kenya na Uganda. Isitoshe lahaja hii ilikuwa ikitumiwa katika biashara za utumwa na biashara zingine za Waarabu. Pia lahaja ya Kiunguja ilikuwa ni lugha nyepesi zaidi kuliko kimvita. Nadharia ya lugha ya Kiswahili 2009.

### **2.4 Lahaja ya Kilibya**

Utafiti huu unahusu uchambuzi wa methali zilizomo katika lugha ya Kiswahili na Kilibya, {moja ya lahaja za Kiarabu}. Tunaposema moja ya lahaja ya lugha ya Kiarabu tunakusudia kwamba ni lugha ya Kiarabu ambayo baadhi ya maneno yake yanatofautiana kimatamshi na uandishi na ile lugha ya Kiarabu fasaha, lakini tofauti hiyo ni ya baadhi ya maneno tu. Hili litaonekana katika methali kadhaa ambazo mtafiti amezichagua katika tafiti hii.

Lakini kwa mfano tu tunaweza kukuonesha hapa baadhi ya maneno ya lahaja ya Kilibya ambayo yanatofautiana kwa lafudhi na maandishi na Kiarabu fasaha ,kwa mfano neno: (نبي) kwa Kilatini tunaweza kuliandika hivi (Nibbiy). Neno hili Walibya hupenda sana kulitumia likimaanisha (Nataka, nahitaji) ambalo kwa yule aliyesomea Kiarabu fasihi akikumbana ghafla na neno kama hili atashindwa kupata



maana hasa ya neno hilo, kwani katika Lugha ya Kiarabu sahihi neno (Nahitaji, Nataka) hutumiwa : (أريد) ambalo tunaweza kuliandika hivi kwa Kilatini (Uriidu). Baadhi ya maneno yanayotumika sana katika lahaja ya Kilibya ni pamoja na:

#### Jedwali Namba 1:Maeneo mnamotumika Lahaja ya Kilibya

Neno kwa lahaja ya Kilibya	Linavyoandikwa kwa herufi za Kilatini	Neno kwa Kiarabu fasihi	Linavyoandikwa kwa herufi za Kilatini	Tarjama yake
باهي	Baahe	تمام	Tamaam	Sawa
هكي	Hekkee	هكذا	Haakadhaa	Hivi
معليش	Maaleesh	عفواً	Af wan	Samahani
خيرك؟	Kheerak	ماذا عندك؟	Maadha in daka	Una nini? vipi wewe?
شينو؟	Sheeno	ماذا	Maadhaa	Kitu gani/ Nini?

Chanzo: Mtafiti, 2013

#### 2.4.1 Asili na Sifa za Lahaja ya Kilibya

Lahaja ya Kilibya ni moja ya lahaja za lugha ya Kiarabu, nayo ni katika lugha za Kisemiti (Munshid Mutlik 2004)<sup>3</sup>. Kisemiti ni kundi la lugha zinazozungumzwa na watu milioni 300 hivi katika Asia ya Magharibi, Afrika ya Kaskazini na Afrika ya Mashariki. Zinahesabiwa kama tawi la lugha za Kiafrika-Kiasia. Wataalamu wa lugha wa Kimagharibi wanaihesabu lahaja ya Kilibya kuwa ni moja kati ya lahaja sanifu za vijijini, na wanaihesabu lugha hiyo kuwa ni miongoni mwa Lugha za Hilaliyah maarufu kama kabila la Bani Suleym bin Mansour, kabila la Waarabu wa zamani sana walioishi Libya. Katika lahaja ya Kilibya herufi (ق qaaf) hutamkwa (Gaaf) kama vile Wamisri wanavyoitamka (جjiim) (Giim) pia herufi (أ alif) huwa wanaitamka (ن nuun) kwa mfano neno (أريد uriidu) huwa wanalitamka (نريد niriid)

<sup>3</sup> Allugha walkitaabal liibiyal kadiima

(نبي nibbiy). Lahaja ya Kilibya inaonekana ni kama kiunganishi kati ya lahaja za Mashariki ya Arabuni, kama vile nchi za Jordan na Guba la Arabuni, pia ni kiunganishi kati yake na nchi za Magharibi ya Arabuni kama Tunisia na Moroco kwa wepesi wake.

Kwa ujumla lahaja ya Kilibya imepwekeka kwa sifa ya wepesi wa kutamka herufi zake, pia kuna sifa kadhaa ambazo lahaja ya Kilibya imesifika nazo, miongoni mwa sifa hizo ni kama kuitamka Qaaf kuwa Gaaf, au kubadilisha namna ya utamkaji wa herufi mbili zinazotokea sehemu moja; kwa kuitamka ile ya pili yenye nguvu na kuificha ya kwanza nyepesi, kwa mfano neno (جنزور Janzuur) hutamkwa (زنزور Zanzuur) au neno (جوزأوزوج Jawz au Zauj) hutamkwa (Zooz).

Pia lahaja ya Kilibya haina maneno mengi ya kigeni; kuna maneno machache ya Kitaliano ambayo hutumika katika vyombo vya majumbani, mfano wa hayo ni kama neno (كاشيك Kaashik : Kijiko) (كوجينا Kojina: Jikoni) (فركييتا Farkiita:; Uma) . Na kuna baadhi ya maneno yaliyotumika kwenye majina ya sehemu kama vile (سبيتار Sabitaar: Hospitali) (جاردينا Gardina: Bostani). Katika lahaja ya Kilibya baadhi ya majina ya vitu huitwa kwa kinyume chake, mfano: Mkaa hutitwa( nyeupe) kipofu huitwa ( mwenye kuona). Lahaja ya Kilibya imesifika kwa kuwa na maneno mengi ya *Kiarabu Fasaha*, hii inatokana na kwamba Walibya hawakuchanganyika na wageni (Wakoloni) isipouwa Waitalia.

## 2.5 Maana ya Methali

Maana ya Methali katika utafiti huu itahusisha vipengele na mkusanyiko wa fikra za watafiti watangulizi na michango yao. Hiyo itampatia mtafiti ufafanuzi wa methali

na kumuwezesha kupata ulinganisho wa pamoja. Hapa mtafiti ameeleza baadhi ya fasili za watafiti waliotangulia na kuchambua baadhi yake, fasili hizo zimekaribiana pamoja na kuwepo tafauti. Uwepo wa tafauti hizo unaonesha pia juhudi za wanalughawiya juu ya umuhimu wa methali na nafasi yake katika jamii. Haraamah (2002) anaeleza kuwa fasili iliyo sawa ni lie ambayo imekusanya mada au kitu kinachokusudiwa kwa pande zake zote, na kuzuia mada au kitu kisichokusudiwa kuingia katika fasili hiyo; fasili inatakiwa iwe imeelezea kinachofasiliwa kwa maneno yenye mipaka maalumu - tarjama ya mtafiti.

Msokile (1992) anasema kuwa, methali ni semi zinazotokana na ujuzi, kanuni na tabia za jamii ambazo kwa kawaida hushauri na kufundisha mambo mbalimbali kwa wanajamii. Methali hufuatilia maisha ya kila siku ya jamii kwa kujihusisha na migongano ama usuluhishi wa masuala mbalimbali katika jamii. Nao Ndugo na Wafula (1993) wanasema kuwa utanzu wa methali ndio utanzu ambao hutumika kwa mapana na marefu katika kutoa maonyo, mafundisho, maadili na kadhalika.

Mulokozi (1989) anaelezea methali kuwa ni semi fupifupi zenye kueleza kwa muhtasari, fikra au mafunzo mazito yatokanayo na uzoefu wa jamii. Fasili hii inaweza ikawa haijitoshelezi kwa kuwa imeibana methali katika kuta ya ufupi (methali ni semi fupifupi...) kwani kuzielezea methali kuwa ni semi fupifupi tu (mfano wa methali hii : **(hasira hasara)** inazitoa zile methali zenye semi ndefu ndefu mfano wa methali hizo ni kama hii: **(Kuku wa mkata hatagi, akitaga haangui, akiangua hutwaliwa na mwewe)** hivyo kwa mujibu wa fasili ya Mulokozi methali ni ile ya kwanza, kwa kuwa ina semi fupi, ama ya pili haitakuwa ni methali

kwa ila ile ya kuwa ndefu. Lakini pia Mulokozi hajaweka mpaka wa ufupi wa usemi anaoukusudia, kwamba uwe na mizani au silabi ngapi.

Vilevile, Mlacha (1981) amelezea dhana ya methali kwa kusema kuwa methali ni mkusanyiko wa ujuzi wa lugha, shuhuda za vitendo na matukio. Fasili hii nayo imeielekeza zaidi methali katika ujuzi wa lugha (ni mkusanyiko wa ujuzi wa lugha) kauli hiyo inaweza kumaanisha kwamba methali ni lazima ifuate kanuni za lugha, kwani ujuzi wa lugha ni neno linalomaanisha iwe fasaha inayoendana na kanuni za lugha.

Pasi na kuangalia ni lugha gani anayoikusudia Mlacha ila kuna methali kadhaa ambazo hazina sifa hiyo, ni zile methali ambazo zipo katika lahaja, na lahaja nyingi hazina kanuni, huwa zinazungumzwa zikitofautiana kimatamshi na kimaandishi na zile za lugha sanifu asilia, mfano wake ni kama methali hii ya Kilibya الليامدور كلافيك (ellee mdaurak laagiik) tarjama yake ni: Ambaye anakutafuta kwa ubaya atakupata. Sasa hapo neon (ellee) kikanuni ya lugha linatakiwa liwe ni (alladhii) ambalo maana yake ni (ambaye) na neno (mdaurak) kikanuni ya lugha linatakiwa kuwa ni (yaduuru alayka) kwa maana ya kwamba: (anayekutafuta kwa ubaya). Sasa kwa maelezo ya Mlacha hii si methali kwa sababu haina utaalamu au ujuzi wa lugha.

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa methali ni semi au kauli zenye busara na mafunzo kuhusu maisha na uhusiano wa watu. Nkwera anasisitiza kuwa methali huwa zinakariri ukweli katika maisha ya mwanadamu katika jamii fulani. Ukweli na umuhimu wa methali yeyote hutengeneza mazingira inamotoka. Hata fasili hii nayo

bado inahitaji maelezo kidogo, tunakubaliana kuwa methali hutoa mafunzo lakini si kwamba methali zote zina busara, kwa fasili ya Nkwera methali kama ifuatayo ya Kilibya inayotumika kumuapiza mtu apate njaa kali adui au yule usiyeelewana naye haiingii katika jamii ya methali, kwani si busara kumuombea mtu njaa, busara ni kumuombea mtu mambo mazuri hata kama ni adui yako. Mfano wa methali isiyokuwa na busara kwa Kilibya:

(جو عالنجوع) (Juu al najuu) tarjama yake ni: Njaa kali, inalingana na methali ya Kiswahili: Adui yako muombee njaa. Mfano wa methali yenye busara kwa Kiswahili: Adui yako mpende. Mfano wa methali ya busara kwa Kilibya: (وعددينعليه) - Waad had deen aleyh) tarjama yake ni: Ahadi ya mtu ni deni kwake: Ahadi ni deni.

Methali ni utanzu ulio tafauti na tanzu nyingine za semi kwani ina sifa mahususi zinazozipambanua. Mtesigwa (1989) ameeleza sifa mahususi za methali kuwa ni;-

- Usemi mfupi wenye urari wa maneno japokuwa maneno hayo si mepesi na ya kawaida.
- Usemi huo ukubalike na watumiaji wa lugha inayohusika hasa kwa sababu;
  - (i) Unalinganisha na kupatanisha vizuri mambo katika hali mbalimbali zinazolenga ukweli ule ule Unatokana na maadili au vitendo vya kila siku vinavyochipuka kutoka katika jamii ya lugha hiyo.
  - (ii) Unaleta maana au unatoa mafunzo mahususi kwa watumiaji wana jamii.

Methali kwa ujumla ni namna au sentensi inayojibiwa kwa midomo yetu pale tunaposukumwa kuwasilisha mambo ya kweli ya kimaisha kwa watu wengine wakati

wa mazungumzo nao kwa hikima za watu wa kale (baba na babu zetu) katika mambo magumu yanayohusu maisha yetu ya kila siku. Ni kwa sababu hii basi tunachagua methali zinazofaa katika jambo fulani na kwa wakati fulani tu. Kwa kuwa methali ni urithi tulioachiwa na watu waliotutangulia na inazingatiwa kuwa ni hazina kubwa ya urithi wa kifikra kwa ajili ya mazingira yetu. Kutokana na ukweli huu tunalazimika kuzama zaidi katika hikima ya methali na kutusukuma katika kina chake ili kupata burudiko ambalo linaingiza utulivu katika nafsi zetu na kunufaika na ujumbe mzuri uliomo ndani ya maana ya methali.

Kwa ufupi methali ni mkusanyiko wa kauli za maneno zilizoko katika sentensi fupi za baadhi ya matukio aliyopitia mwanadamu na kuchuja ndani yake mambo yenye kuathiri na mawaidha. Mara nyingi methali hubeba na kuonesha mapitio ya matukio na visa na wale wanaohusika na matukio hayo. Ni kwa sababu hii basi watu wa jamii na lugha mbalimbali hawajaridhia kupuuza au kusahau matukio, hivyo kuyasajili katika maneno ambayo watu huyanukuu zamu kwa zamu, tukio kwa tukio na hata kizazi baada ya kizazi ili kulea na kutunza vizazi hivyo visipotee, na ndio maana methali kama haraka haraka / haina Baraka/tamaa mbele mauti nyuma/ penzi ni majani, mapenzi ni maua popote huchanua n.k. zimerithishwa tokea enzi za wahenga na wahenguzi mpaka leo hii.

Hivyo, kutokana na fasili na sifa zitolewazo mtafiti anafasili methali kuwa ni (*Semi-elekezi maalumu “fupi au ndefu” kuhusu maisha zinazotokana na tajiriba*) tunaposema zinazotokana na tajiriba tunamaanisha kwamba ni zao la hekima inayotokana na maisha aliyoishi binadamu, kwani hakuna methali ambayo iliwahi kusemwa kabla ya tukio maalumu ambalo ndiyo tajiriba iliyomfanya mhusika

atamke hekima hiyo. Ila jambo pekee ambalo linakuwa si rahisi kuligundua kwa mara moja ni kwamba je tukio hilo linakumbukwa au halikumbukwi?

Kama tukio hilo linakumbukwa basi hilo lina umuhimu wake, lakini hata kama itatokea kwamba tukio hilo halikumbukwi inatakiwa ieleweke kuwa hekima kwa maana ya methali ile itabaki ikitumiwa na watu wa jamiile au hata kwenda kwenye jamii nyingine, ni kwa sababu ya umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Hii inatokana na ukweli kwamba hekima, elimu na methali ni zawadi ambayo haina ulazima kujua inatoka wapi, bali huangaliwa umuhimu wake katika kuendeleza uutu na utukufu wa binadamu.

Kwani si rahisi kuamini kwamba methali zinazotumika katika lugha ya Kiswahili ambazo zinafanana na zile za Kilibya au na za nchi nyingine yoyote duniani ziwe na matukio tofauti, yamkinika kuwa tukio la methali hiyo lilikuwa ni moja tu na lilitokea katika ima jamii ya Kiswahili au ya Kilibya au ya nchi yoyote, ila nchi nyingine baada ya kuona umuhimu wa methali ile ikajiona inaichukua pasi na kuangalia sababu ya tukio-semwa, ni kwa sababu ilizingatia zaidi faida ya methali na si msemaji au tukio la methali.

Nsookwa (2011) anasema akinakili kutoka kwa (Finnegan, 1970): Habari ya kugundua nyakati za utungaji methali fulani inaweza kupatikana katika methali zenyewe pengine zinataja majina ya watu wakuu wa zamani. Kwa mfano, methali ya Kiganda isemayo: ‘Ontuuse Nalunga yatuuka Jjuuko’ inataja mwanamke aliyeolewa na kumfaa sana mfalme mmoja, Jjuuko wa Ufalme wa Waganda. Kinachohitajika hapa ni kujua ni wakati gani kihistoria ambapo Jjuuko alikuwa

mfalme. Hatimaye mtafiti anaweza kukisia miaka au nyakati za kutokea kwa methali yenyewe kulingana na historia.

Lakini ni wazi kwamba kuna methali chache sana zinazobashiri wakati wa kubuniwa kwake. Kwa sababu hiyo, hakuna kabila linalotaja watungaji wa methali zake au methali kwa jumla ingawa zinatumika sana katika usimulizi wa ngano. Hata kwa wakati wa kisasa hakuna anayeweza kudai miliki ya utunzi wa methali fulani au kuanza maandishi ya orodha ndefu ya methali alizobuni yeye mwenyewe. Kwa hivyo hapawezi kutokea ushahidi wa kuona methali ikiundwa.

Methali zilizo nyingi hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kudokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yanayotokana na tajiriba ya jamii husika. Mulokozi (1996) ameeleza kuwa, kutokana na ufupi na usanii wake, methali zinaweza kutoa mwongozo au mafunzo kwa mafanikio zaidi kuliko maelezo ya kawaida.

Mulokozi (1996) anaendelea kusema kuwa, methali ni utanzu ambao hutegemea kuwepo kwa fani nyingine, kwa mfano, maongezi au majadiliano mazito katika miktadha maalumu ya jamii. Mfano; Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu'; au 'Mtoto akililia wembe mpe'. Methali hizi hutumika katika mazingira ya mazungumzo yenye lengo la kumuonya mtu mkaidi kuhusu athari ya jambo.

## **2.6 Fani katika Methali**

Kifani, methali ni usemi wenye muundo wa sehemu kuu mbili. Wafura na Ndungo (1993) wamebainisha kuwa, methali nyingi huwa na sehemu ya kwanza ambayo



huanzisha wazo na sehemu ya pili, hukanusha au kukamilisha wazo hilo. Mfano wa methali hizo ni kama zifuatazo:

<b>Sehemu A</b>	<b>Sehemu B</b>
Dunia ikikupa ngono,	kila utendalo nono.
Baada ya dhoruba,	huja utulivu
Mgaagaa na upwa,	hali wali mkavu
Mfuata nyuki,	hakosi asali

Katika methali ya kwanza na ya pili fungu (A) linaonesha wazo anzilishi wakati sehemu (B) inaonesha ukamilifu wa wazo hilo. Ama methali ya tatu na ya nne sehemu (A) inaonesha wazo-anzilishi wakati sehemu (B) ya methali hizo inakanusha. Muundo huu pia unapatikana katika methali za Kilibya, hebu tusome methali zifuatazo:

<b>Sehemu (A)</b>	<b>Sehemu (B)</b>	<b>(ب)</b>	<b>(ا)</b>
Almktoub baayin min un waanah	المكتوب باينمنعوانه		

<b>Kilichondikwa</b>	<b>kipo wazi juu ya anuani yake</b>
Almldough yat khaayalil habal	الملدو غيتخايلالحبل

<b>Aliyegongwa na nyoka,</b>	<b>kamba huidhania kuwa ni nyoka</b>
elliyad brouha mat swaffag	الليدير وحاتماتصفق

<b>mkono mmoja</b>	<b>haupigi kofi</b>
Ellee maa yaakul bi iidah maa yashb	الليماياكلبيدهمايشبع

<b>asiyekula kwa mkono wake,</b>	<b>hashibi</b>
----------------------------------	----------------

Lakini zipo pia methali ambazo wazo-anzilishi lake lina sehemu mbili, na jawabu lake la kukamilisha wazo hilo au kukanusha pia lina sehemu mbili. Mfano wa hizo ni kama zifuatazo:

<b>Sehemu ya kwanza</b>		<b>sehemu ya pili</b>	
<b>(wazo-anzilishi)</b>		<b>(ukamilishaji/</b>	
<b>ukanushaji wa wazoanzilishi)</b>			
<b>(A)</b>	<b>(B )</b>	<b>(A)</b>	<b>(B)</b>
Dau dogo	huambaa mwambao	kubwa	huenda penye kilindi
Jinga	ni lako mwenyewe	la mwenzio	huwezi kulitumia
Lako,	lako peke yako	ukifikiwa	lina wenzio

Methali zenye muundo huu, mara nyingi hutumika kama dokezo katika mazungumzo. Ni kumaanisha kwamba mzungumzaji hutaja sehemu A na B ya wazo-anzilishi na akamwachia msikilizaji sehemu A na B ya pili kukamilisha au kukanusha wazo. Mulokozi amesema kuwa baadhi ya methali huwa na muundo wa kinudhumu (kishairi). Methali hizo huwa na urari na mizani na pengine mpangilio maalumu wa vina. Mfano aliolea ni; Haraka haraka haina baraka' Wamitila (2011) anasema katika sanaa ya Kiswahili sanaa zote mbili<sup>4</sup> zinasimamia mtindo wa ubeti wa shairi kwa vile huwa na mstari unaogawika sehemu mbili, moja ikitegemea nyingine.

Wamitila anaendelea kueleza kuwa: Kila mstari katika ubeti hugawika kwa vipimo sawa vya mizani kulingana na mistari mingine. Kwa hiyo tunapata kwa mfano, shairi

---

<sup>4</sup> Vitendawili na methali

lenye mizani 16 ; yaani kila mstari una silabi 16 na kila mstari una vipande viwili vya mizani nane nane( 8 :8) methali ya Kiswahili ina mtindo huu huu pia ; lakini tofauti na shairi, methali za Kiswahili zina mstari mmoja tu unaogawika sehemu mbili zenye mizani sawa au zinakaribiana vipimo. Sehemu hizo za mgawiko huwa zinakamilishana kimaana katika kile tunachoweza kukiita KISABABISHO na MATOKEO. Hii hapa baadhi ya mifano inayopatikana katika kamusi ya methali.

<b>KISABABISHO</b>	<b>\</b>	<b>MATOKEO</b>
1 Mtaka cha mvunguni (Mizani 8)		sharti ainame (Mizani 7)
2 Haraka haraka (Mizani 6)		haina baraka (Mizani 6)
3 Mwenda tezi na omo (Mizani 7)		hurejea ngamani (Mizani7).

Tunaweza pia hapa kuweka methali kama:

4 Haba na haba (Mizani5)	hujaza kibaba' (Mizani6)
5 Masikini akipata (Mizani8)	matako hulia mbwata' (Mizani8)
6 Hamna hamna (Mizani6)	ndimo mliwamo (Mizani6)

Katika urari wa vina tunaona methali 5,4 na 2 zinafanana vina, wakati katika methali ya 6,3,5 na 6 kuna usawa wa mizani. Ama methali ya 1 na ya 4 hizo ni zile methali zenye ukaribu wa mizani. Vilevile, Mulokozi na Wafura na Ndungo (1993) wamebainisha kuwa, methali zilizo nyingi huelezwa kwa kutumia tamathali hasa

sitiari na mafumbo. Sitiari ni mbinu ya kutumia dhana moja kuwakilisha dhana nyingine isiyohusiana nayo. Mathalani Nuru huwakilisha ukombozi, Kiza huwakilisha kitisho.

Nsookwa ananakili akisema: Mwanaisimu mashuhuri Walpole (1941) naye alichangia maana ya dokezo za sitiari kwa kuunda nadharia ya uhamishaji maana yenye msingi wa sitiari. Kwake, sitiari ni kuazima jina la kitu kingine. Kwamba, sitiari ni kipengele cha kila lugha na kwa hivyo matumizi ya sitiari yalianza na chanzo cha lugha au matumizi ya maneno katika lugha yoyote; kuigiza sitiari ni kwa zamani za kale tangu chanzo cha maisha ya binadamu. Alisema kwamba kutoka chanzo cha dunia binadamu wa kila mbari walitambua umuhimu wa kutumia kumbukumbu zao kuhusu kitu fulani kutafakari kitu kingine kwa njia ya kuvimithilisha. Kwa jambo hilo, Walpole (1941) aliunda nadharia ya uhamishaji maana yenye kanuni ifuatayo: Katika msembo wenye sitiari, ishara hurushwa kutoka muktadha mmoja kwenda mwingine ulio tofauti kabisa lakini katika msingi wa kumithilisha vipengele vilivyomo katika miktadha hiyo miwili. Jambo hii limefafanuliwa wazi na mchoro ufuatao kutoka kwa Walpole.

Kielezo hiki cha Walpole kinaeleza nadharia ya uhamishaji maana wenye msingi wa sitiari. Mchoro huu unaonyesha namna matumizi ya sitiari yanavyomithilisha miktadha miwili iliyo tofauti katika methali moja. Mchoro huo unathibitisha kwamba wahusika upande wa A wanalingana na wahusika upande wa B kwa kutegemea nguvu za mfanano. Kwa hivyo, msemaji (P) katika A anatumia ishara ya lugha (L) kwa muktadha (T) kupokelewa katika B (C). Mishale katika pembetatu inathibitisha


kwamba kuna mawasiliano kamili baina ya C na P. Kwa kifupi sitiari ni kufananisha vitu viwili vinavyofanana katika sifa fulani nakutofautiana katika sifa nyingine pasi na kutumia neno (kama) methali za Kiswahili zifuatazo zina methali zenye istiara:

Elimu bahari

Ukubwa jalala

Dunia tambara bovu

A



**Kielezo Namba 2: Nadharia ya Uhamishaji Maana**

**Chanzo: Nsookwa**

Muktadha

P = Msemaji au mwandishi

L = Lugha ishara/sitiari

C = Wasikilizaji au wasomaji

Mtesigwa, (1989) anazona methali kuwa ni mojawapo ya fani zinazotumia sanaa mahususi ya fasihi katika kuipa lugha uhai na pia kutekeleza kazi ambazo hutazamiwa zitendwe na fasihi. Balisidya, (1987), yeye anaona kuwa methali kama ni misemo itumiwayo kueleza kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili kutoa maadili au maonyo fulani. Misemo hii humilikisha maisha kwa njia ya tamathali, picha na

ishara. Wangari na Ndungo (1991) wameeleza kuwa dhima kuu ya methali hujitokeza katika malezi. Methali zimejaa maadili ambayo humsaidia mwanadamu na kumwongoza kwenye msingi bora wa maisha. Huweza kuwa masuto au maadili yenye lengo la kuonya<sup>5</sup>, kuusia,<sup>6</sup> kushauri na kufunza<sup>7</sup>. Methali za masuto huwa na

---

<sup>5</sup> Mfano wa methali za kuonya za Kiswahili zifuatazo:-

- 1 Dulu liumalo silipe kidole
  - 2 penye kuku wengi usimwage mtama
  - 3 Asiyeangalia huishia ningalijua
- Hata katika methali za Kilibya kuna methali zenye lengo hilohilo nazo ni kama zifuatazo:
- 1 ما تُضْرِبْ لِكَلْبٍ نَيْنَ تَعْرِفْ مَوْلَاهُ  
Maa tudhrb lakalab nein taarif mawlaah  
Usimpige mbwa mpaka umjue mwenyewe
  - 2 اللي اديره في خوك .. ايديره فيك الزمان  
Ellee tdiyrh f khuuk, idiir fiik zmaan  
Unalomfanyia mwenzako, nawe zama zitakufanyia
  - 3 مَثْوَرِي عَشَّكَ لِلطَّيُورِ لِيَخْرَبُوهُ  
Matwarri ash shak lityuur liikharbuuh  
Kiota chako usiwaoneshee ndege, watakiharibu

<sup>6</sup> Mfano wa methali za kuusia ni kama zifuatazo:

- 1 Ala! Ala! Jirani kama ndugu mli kule  
Ala: shime; pataneni. Mli: mkiwa
- 2 Radhi ni bora kuliko mali
- 3 Msitukane wakunga na uzazi ungalipo

Na kwa kilibya kuna methali za kuusia, zifuatazo ni baadhi ya hizo:-

- 1- الجار قبل الدار  
Al jaar gabla ddaar  
Jirani kwanza kabla ya nyumba
- 2- ضيف ليله مَثْوَرِيَه ففرك

lengo hilo lakini maneno yake huwa ya kukaripia na wakati mwingine kukemea. Maneno ya aina hii huwa ni makali kwa masikio na katika lugha ya kawaida huonesha dalili za utovu wa heshima au lugha ya adabu. Maneno haya mara nyingi huwa hayatumiki katika halaiki au mbele za watu wazima na wageni.<sup>8</sup>Mwai na

---

Dheif leelah matwarriih fagrak

Mgeni wa usiku mmoja, usimuoneshee umasikini wako.

3- عليك بابنات لوصول راء الزمان بطول

Ala! Ala! Mabinti walolelewa, hao ndio msaada wako baadae.

Methali hii huusiwa mtu anayetaka kuoa.

<sup>7</sup> - mfano wa methali za kushauri na kufunza katika kiswahili ni kama zifuatazo:

1 heri kujikwaa mguu kuliko ulimi

2 epuka maovu nayo yakuepuke

3 ajuaye mengi hasemi mengi

Na katika Kilibya ni kama methali zifuatazo:

1- البنادم تربطه كلمته

Albanaadam turbut huu kalmatah

Binadamu hufungwa na kauli yake

2- بات اعلى غيظ أولى اعلى تبات على اندامه

Baat alaa gheedh oulaa alaa tbaat alaa n-daamah

Ni bora ukalala ilhali umekasirika kuliko kulala na majuto.

3- إن كان الكلام من فضة فإن السكوت من ذهب

Inkaanal kalaam mi fidhwa fainna ssukuut mi dhahab

Kama kuzungumza kunaokanana fedha basi kunyamazakunatokana na dhabu.

<sup>8</sup> Katika methali ambazo ni aibu kuzizungumza mbele ya halaiki ni kama hizi methali za Kiswahili zifuatazo:

1 Nyani haoni kundule

2 Nyege kunyegezana

3 Usinyie kambi, huenda ukauya papo

Ndungo wanaendelea kueleza kuwa, aina hizi mbili za methali huwa zinalenga ukweli wa maisha; zinapotolewa huwa zimekusudia kutoa maonyo, mafundisho na kusaidia kurekebisha tabia fulani za watu wa jamii inayohusika. Malezi yaweza kufanikiwa kwa kutumia lugha nzuri au lugha kali. Kwa njia ya methali, tabia za watu zaweza kukaripiwa na kurekebishwa. Dhima kuu ya methali ni kufunza na kulea mtu ili aweze kulingana na matakwa ya jamii yake.

Katika kazi hii, itabainika kwamba lugha hupambwa na tamathali za usemi, methali zikiwemo. Tamathali hizi huhamisha maana. Uhamishaji huu wa maana ni mbinu ya kuibua maana ya kiashiria kutokana na maana ya kiashiria kingine. Mtafiti amegundua kuwa hakuna kazi iliyochunguza kufanana na kutafautiana kwa methali za Kiswahili na za Kilibya katika dhamira ya elimu, malezi, kujali chako, maonyo na tahadhari. Mtafiti hawezi kudai kwamba hakuna kazi iliyowahi kufanyika katika methali-linganishi kati ya methali za Kitanzania na nchi nyingine, hapana, kwani kazi tangulizi kama ile ya tafiti linganishi kati ya methali za Kitanzania na Kikorea inayopatikana katika Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, na kazi ya Ahmed Alsanousi katika methali, ni juhudi tangulizi ambazo zimetoa mwangaza wa kazi zifuatazo zinazojihusisha na utanzu wa methali, lakini kazi hizo hazikugusia hata kidogo dhamira zilizochaguliwa na kazi hii, kama ambavyo zimeacha uchambuzi muhimu katika mambo ya kifani ambayo mtafiti atayaorodhesha hapo baadaye. Hivyo, utafiti huu unategemewa kuziba pengo la utafiti ambao aghalabu haujawahi kufanywa.

---

<sup>8</sup> Kufa kwa mkundu mavi hutawanyika



## **2.7 Hitimishi**

Sura hii imefanya upitiaji wa kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti ili kuona watafiti watangulizi wanazungumza nini kuhusiana na mada yetu ya utafiti. Kwa ujumla kazi tangulizi zinaonesha kwamba hakuna utafiti wa kina ambao tayari umeshafanyika katika kulinganisha na kutofautisha methali za Kiswahili na zile za Kilibya na huu ndio utafiti wa kwanz kulifanya hilo. Sura inayofuata inazungumzia nadharia mbalimbali za uhakiki wa kifasihi.

## **SURA YA TATU**

### **3.0 NADHARIA ZA UHAKIKI WA FASIHI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inapitia nadharia kadhaa ambazo kwanzo zimetumika katika kuuhakiki methali za Kiswahili na zile za Kilibya. Ni vema ikaeleweka wazi kwamba, uhakiki ama utafiti wowote ule wa kifasihi ni lazima uongozwe na nadharia muafaka ili uweze kutoa majibu yanayokidhi malengo ya utafiti kama yalivyoorodheshwa na mtafiti. Nadharia ndiyo itoayo mwelekeo wa utafiti; njia, mbinu, upitiaji wa kazi tangulizi na uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti wote hufanywa kwa kuongozwa na nadharia zilizoteuliwa na mtafiti. Kwa msingi huu utafiti huu umeongozwa na nadharia za Simiotiki, Umarx, Dhima na Kazi, Uamilifu na Umuundo. Maelezo ya kina kwa kila nadharia yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

#### **3.2 Nadharia ya Simiotiki**

Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuihakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Wamitila, 2002:132).

Ishara zinazojitokeza katika kazi za fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Chandler (1992) anaeleza kwamba, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa alama hizo.

Wasomaji na watazamaji wa kazi za fasihi hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama hizo. Mawazo haya yanakamilishwa na yale ya Chandler (1992) aliposema kuwa, tunafikiri kwa kutumia alama. Alama hizo zinakuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na mtenda au yambwa. Anaendelea kueleza kwamba, kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakiifasiri kama kirejeelee, yaani kinasimama kwa niaba ya kitu kingine badala ya chenyewe.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja (a signifier), yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejeelee (a signified), yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja, na kirejeelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejeelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao. Bathes (1994) akaja na aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa Kinatukio, Kihemenitiki, Kiseme, Kiishara na Kiurejeeleezi.

Methali za Kiswahili na zile za Kilibya hutumia lugha ya picha, ishara, taswira na sitiari ambazo humlazimu mtafiti kuwa na taaluma ya uchambuzi wa Kisimiotiki ili aweze kuchambua kazi yake kwa ufasaha. Hivyo basi, nadharia ya Simiotiki ilikuwa muhimili mkubwa katika kuhakiki methali za Kiswahili na zile za Kilibya kutuwezesha kubainisha dhamira mbalimbali katika methali husika.

### 3.3 Nadharia ya Umarx

Msingi mkubwa wa nadharia hii unatokana na mawazo ya Karl Marx na Fredrich Engels. Karl Marx (1818-1863) anahusisha U-Marx na Nyanja kama vile uchumi, historia ya jamii na mapinduzi (Wamitila, 2002:182). Kimsingi, mawazo ya Marx yanalenga kuwataka wanafasihi kuzitazama hali za jamii zao zilivyo na kuzitafutia ufumbuzi kwa maana ya kuzibadilisha kuliko kuzitafsiri tu.

Mawazo ya Karl Marx kuhusu historia na miundo ya kijamii yana nafasi kubwa katika nadharia hii. Umarx ni falsafa ya Kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Umarx hautegemezi mfumo wake wa kifalsafa kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali kwenye uhalisi unaonekana (Wamitila, 2002:182). Mfumo wa maisha tulio nao leo ni ule ulioongeza tofauti kati ya walionacho na wasio nacho (utabaka) na kusababisha kuwapo kwa mgogoro wa kitabaka katika jamii za Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Kupitia migogoro ya kijamii ndipo masuala mbalimbali ya kijamii yanapojitokeza na kusawiriwa kupitia methali za Kiswahili na zile za Kilibya. Wamitila (2002:183) anaeleza kwamba:

*Wahakiki wa Ki-Marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi – jamii. Itakumbukwa kuwa Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka .... Kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mambo mengine.*

Mambo haya ndiyo humfanya binadamu kupambana ili aweze kuyapata na kisha aweze kuishi maisha mazuri. Wakoloni kwa hakika hawakutoa fursa kwa wananchi kuwa na maisha mazuri kwa kuwa daima wakoloni waliwatumikisha kwa kazi nyingi malipo kidogo. Hali hii iliwafanya wananchi kufanya kila linalowezekana ili waipate haki yao ya uhuru na kisha kupanga mipango yao ya maendeleo itakayowaletea maendeleo. Hivyo basi, nadharia ya Umarx imeongoza vema uchambuzi na uhakiki wa methali za Kiswahili na Kilibya kama inavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu hii.

### **3.4 Nadharia ya Dhima na Kazi**

Kwa kuanzia mtafiti atatoa maelezo juu ya nadharia ya dhima na kazi ambayo inahusishwa na mwanafalsafa Sengo (2009). Nadharia hii imezichambua kazi za fasihi kwa kuangalia kazi na dhima kwa kila kipengele cha fasihi. Mtafiti atatumia nadharia hii kuzichunguza methali za Kilibyana Kitanzania ili kubaini dhima na kazi za vipengele vya fasihi. Aidha nadharia hii ina kiangalia kipengele cha lugha kwa kutilia mkazo kuzingatia kila kijenzi cha lugha.

### **3.5 Nadharia ya Uamilifu**

Nadharia hii pia inashikilia kuwa kila kitu duniani kina kazi yake. Na kuwa kazi mbalimbali katika mfumo mmoja ndiyo zinazokamilisha kazi nzima ya huo mfumo. Kwa mfano, ikiangaliwa mwili wa mwanadamu, itabainika kuwa viungo mbalimbali vya huo mwili kila kimoja kina kazi maalum. Miguu ina kazi yake maalumu, hivyo hivyo mikono, kichwa, tumbo, na kadhalika. Ingawaje kila kiungo kina kazi maalumu tofauti na kazi ya kingine, ila vyote vnafanya kazi ya kuutumikia mwili. Mfano huo ni sawa na vijenzi vya lugha ya kifasihi kama ilivyo.

### **3.6 Nadharia ya Umuundo**

Nadharia hii inahusishwana mawazo ya mwanafalsafa na mwanalughawiya Mswisi, Ferduand de Saussure. Umuundo unatilia msisitizo zaidi muundo wa kazi ya fasihi. Mtazamo wa kimuundo au kimfumo wa kilughawiya ndiyo uliowaathiri wahakiki wa kimuundo na kuiona kazi ya fasihi kama muundo tu. Kwa mtazamo huu mtunzi hapewi nafasi. Wana muundo wanaiona kazi ya fasihi kuwa imepangwa kama lugha tu. Aidha, wanamuundo wanaamini kuwa kazi ya fasihi kama hii ya methali inayoshughulikiwa na utafiti huu, haina urejelezi. Kutokuwa na urejelezi huko ndiyo sababu wanamuundo huwazia zaidi lugha inayotumika kuiundia kazi ya fasihi. Wanamuundo wanaamini kuwa neno halina haja ya urejelezi kwa ajili ya kupata maana. Kwa wao lugha ni mfumo unaojitosheleza. Ni mfumo usiotegemea lengo la msanii wa kazi.. Maana ya haya ni kuwa nadharia hii inajali na kujishughulisha zaidi na maana inavyopatikana au kukuzwa kuliko maana yenyewe. Mtafiti ataitumia nadharia hii pia kuchunguzia methali za Kilibya na Kitanzania ili apate kuona namna lugha inavyotumika na methali hasa katika ujenzi wa dhanna zake.

### **3.7 Hitimishi**

Sura hii imeeleza juu ya nadharia mbalimbali ambazo zimetumika katika kufanya uhakiki wa methali za Kiswahili na zile za Kilibya kam zilivyowasilishwa na kuchambuliwa katika sura ya tano ya tasnifu hii. Miongoni mwa nadharia zilizowasilishwa ni pamoja Simiotiki, Umarx, Dhima na Kazi, Uamilifu na Umuundo. Sura inayofuata inawasilisha mbinu mbalimbali za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti wetu.

## **SURA YA NNE**

### **4.0 MBINU ZA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Utafiti ni taaluma ya kisayansi inayotumika katika kulisoma, kulichunguza na kulitafiti jambo ili kupata data aidha kwa ajili ya kutatua tatizo fulani ama kuongeza maarifa na ujuzi juu ya jambo husika (Kothari, 2008). Ili kuwezesha azma ya utafiti kufanikiwa ni wajibu kwa mtafiti kuanda mbinu mbalimbali za utafiti ambazo atazitumia katika kukusanya data za utafiti husika. Kwa kuwa utafiti huu nao ni wa kitaaluma mtafiti amelazimika kuandaa mbinu mbalimbali za utafiti kama zinaainishwa hapa chini.

#### **4.2 Usanifu wa Utafiti**

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unaoonesha namna na jinsi utafiti utakavyofanyika ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika (Kothari, 2008). Utafiti huu umetumia mbinu ya usanifu ijulikanayo kama uchunguzi kifani katika kukusanya data. Yin (1994) anasema kwamba, uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambapo mtafiti huteua sehemu au jambo au kitu maalumu ambacho atakifanyia utafiti kati ya vingi vilivyopo ili aweze kukidhi mahitaji ya utafiti wake. Katika utafiti huu, methali za Waswahili waishio Dar es Salaam na za Walibya ndiyo zilizoteuliwa na kufanyiwa utafiti wa kina. Mbinu hii ya usanifu ni muafaka katika utafiti huu kwa sababu inatoa fursa kwa mtafiti kulitafiti jambo moja kwa muda wa kutosha na hivyo kupata majibu sahihi ya maswali ya utafiti (Robson, 2007). Vilevile, mbinu hii humuwezesha mtafiti kuzama na kulitafiti jambo moja kwa undani kabisa na kisha kulitolea mahitimishi stahiki (Cresswel, 2009). Kothari

(2008) anasema kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuufanya utafiti wake kwa gharama nafuu.

### **4.3 Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu umekusanya data za aina mbili ambazo ni data za upili na za msingi. Data hizi ni muhimu katika kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti wetu na hatimaye lengo kuu la utafiti. Tunaanza kutoa maelezo juu ya data za upili.

#### **4.3.1 Data za Upili**

Data za upili ni aina ya data katika utafiti wowote ule wa kitaaluma ambazo hukusanywa kutoka katika maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti (Kothari, 2008). Madhumuni hasa ya kukusanya data hizi ni kujaziliza data za msingi ili kusaaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Data hizi hukusanywa kutoka katika vitabu, makala, majarida, tasinifu, magazeti, tovuti na wavuti. Ili kuweza kuzipata data hizi mtafiti alilazimika kwenda maktaba mbalimbali kutafuta maandiko yanayohusiana na mada yake na utafiti na kuyasoma kwa kina. Miongoni mwa maktaba alizozitembelea ni pamoja na Maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Maktaba na Makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Maktaba ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar na Maktaba Kuu ya Taifa.

#### **4.3.2 Data za Msingi**

Data za msingi kwa kawaida huwa ni data ghafi ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti kwa ajili ya kujibu maswali yake ya utafiti na hazijawahi



kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama huu unaokusudiwa kufanywa hivi sasa (Kothari, 2008). Data hizi hukusanywa masikanini kutoka kwa watafitiwa mbambali walioteuliwa na mtafiti na ambao anatambua kwamba watampatia data muafaka zitakazosaidia kujibu maswali yake ya utafiti. Data hizi pia hukusanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali ambazo tumezianisha hapa chini.

#### **4.3.2.1 Usaili**

Usaili ni mbinu ya kukusanya data za msingi kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana baina ya mtafiti na watafitiwa-ambapo mtafiti huuliza maswali aliyoyaandaa kwa watafitiwa wake. Watafitiwa hutoa majibu huku mtafiti akiyanukuu katika shajara maalumu aliloliandaa (Kothari, 2008). Mbinu hii ni nzuri katika utafiti kwa sababu inatumia muda mfupi kupata data nyingi zinazojibu maswali ya utafiti. Methali nyingi zimepatikana kwa njia ya usaili wa ana kwa ana kwa kuhoji watu mbalimbali kutoka wilaya hadi wilaya. Jumla ya watu 50 walio na umri kati ya miaka 46-90 na watu 100 kati ya 18-45 walihojiwa na kutoa data zilizofanikisha utafiti huu.

#### **4.3.2.2 Hojaji**

Hojaji ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambapo mtafiti huandaa maswali katika karatasi huku akiacha nafasi za kujazwa majibu na watafitiwa wake (Kothari, 2008). Kupitia njia hii mtafiti hutawanya hojaji zake kwa watafitiwa wake na kuziacha ili wajaze ndipo huja kuzikusanya baadaye. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba, mbinu hii ni nzuri kwa sababu wakati watafitiwa wameachiwa hojaji wajaze, mtafiti huendelea na jambo jingine linalohusiana na utafiti wake. jumla ya hojaji 80 zilijazwa na

watoto wa shule za msingi darasa la sita na la saba wenye umri kati ya miaka 10-17.

Vile vile, hojaji 20 ziilijazwa na vijana wenye umri kati ya miaka 18-45.

#### **4.3.2.3 Ushuhudiaji**

Ushuhudiaji ni mbinu ya ukusanyaji wa data za msingi ambapo mtafiti pamoja na msaidizi wake kushuhudia moja kwa moja jambo walilokusudia kwa ajili kuliona namna lilivyo ama linavyotendeka na kisha kukusanya data za utafiti wao (Babbie, 1999). Mbinu hii ni nzuri kwa sababu inasaidia kukusanya data halisi kama zinavyotokea katika muktadha halisi na hakuna uwezekano wa kudanganya ama kupata data zisizo halisi ama sahihi. Kupitia mbinu hii mtafiti alitembelea katika maeneo ya vijiwe vya vijana na vile vya wazee ili kubaini aina ya methali wanazotumia katika mawasiliano yao. Katika vijiwe hivyo mtafiti aliweza kukusanya methali mbalimbali na kuupata muktadha mzima wa matumizi yake.

#### **4.4 Sampuli na Usampulishaji**

Utafiti wowote ule wa kitaaluma hauwezi kufanywa kwa mtafiti kuitafiti jamii yake yote kwa wakati mmoja kwa sababu muda hauwezi kuruhusu hilo lifanyike. Kutokana na ukweli huu mtafiti hulazimika kuteua sampuli ndogo ambayo itawakilisha jamii nzima ili kutimiza madhumuni mahususi ya utafiti wake. Kwa maana hiyo basi, sampuli ni wawakilishi ama viwakilishi vya watafitiwa wote ambavyo huteuliwa na mtafiti ili vimpatitie data lengwa za kumilisha utafiti husika. Ili mtafiti aweze kupata sampuli husika ni lazima afanye usampulishaji. Kumbe basi usampulishaji ni kitendo cha kuteua wawakilishi wa watafitiwa katika utafiti (Babbie, 1999). Zipo aina mbalimbali za sampuli ambazo hutumiwa katika utafiti japo katika utafiti huu tumetumia sampuli nasibu na lengwa.

#### 4.4.1 Sampuli Nasibu

Robson (2007) anaeleza kwamba, sampuli nasibu ni ile ambayo watafitiwa huteuliwa kinasibu kwa maana kwamba kila mtafitiwa ana nafasi sawa na mwingine katika kuteuliwa kushiriki katika utafiti. Aina hii ya sampuli imetumika katika utafiti wetu pale ambapo tumeteua watoto wenye umri kati ya miaka 10-17 na kuwapatia hojaji. Kila mtoto mwenye umri tajwa hapo juu alipewa fursa sawa na mwingine katika uteuzi wa wawakilishi. Jumla ya watoto 80 kwa kuzingatia jinsi walijumuishwa katika utafiti huu. Vile vile, watu wazima ambao bado hajafikia umri wa uzee nao tuliwateua kupitia mbinu hii. Jumla ya watu wazima 100 kwa kuzingatia jinsi walijumuishwa katika utafiti huu Maelezo zaidi kuhusu hili yanaonekana katika jedwali namba 2 hapa chini.

#### 4.4.2 Sampuli Lengwa

Hii ni aina ya sampuli ambayo huteuliwa na mtafiti kwa imani kwamba ni muafaka na itampatia data anayoihitaji katika utafiti wake. Aina hii ya sampuli imetumika kuwateua wazee ambao mtafiti aliamini kwamba watampatia data sahihi zilizojibu maswali yake ya utafiti. Jumla ya wazee 50 kwa kuzingatia jinsi waliteuliwa kupitia sampuli lengwa. Maelezo zaidi kuhusiana na suala hili yanaonekana katika jedwali namba 2 hapa chini.

**Jedwali Namba 2:Sampuli ya Watafitiwa na Idadi yao**

Na.	Waliosailiwa/Kuhojiwa	Jinsia	Umri (Miaka)			Jumla
			10-17	18-45	46 -90	
1.	Watoto	ME	40			40
		KE	40			40
2.	Watu wazima	ME		60		60
		KE		40		40
3.	Wazee	ME			20	20
		KE			30	30
<b>JUMLA</b>			<b>80</b>	<b>100</b>	<b>50</b>	<b>230</b>

**Chanzo: Mtafiti, 2013**

Mbali na uteuzi huo mtafiti ameteuwa kutoka katika kundi la wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kilibya. Uteuzi huo usiokuwa wa kishabaha ulifanyika huku kigezo cha jinsia kikitumika. Kwa kufanya hivi mtafiti atakuwa na jumla ya watafitiwa 100 katika kila lugha. Muhtasari wa uteuzi utakaoteuliwa umeoneshwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Namba 3:Wazungumzaji wa Kiswahili na Kilibya**

Lugha	Jinsia		Jumla
	Me	Ke	
<b>Kiswahili</b>	25	25	50
<b>Kilibya</b>	25	25	50
<b>Jumla kuu kwa wahojiwa wazugumzaji wa lugha zote</b>			<b>100</b>

**Chanzo:Mtafiti, 2013**

#### **4.5 Vifaa na Zana za Utafiti**

Vifaa na zana za utafiti ni nguzo muhimu katika kufanikisha utafiti husika. Katika utafiti huu tumetumia vifaa na zana mbalimbali kama zinavyoainishwa hapa chini.

##### **4.5.1 Kalamu na Karatasi**

Kalamu na karatasi ni vifaa muhimu katika ukusanyaji wa data. Kalamu imetumika katika kudondoa na kunukuu maelezo yaliyotolewa na watafitiwa ambayo ndiyo sehemu ya data za utafiti wetu. Karatasi imetumika kama sehemu ya kudondolea maelezo kutoka kwa watafitiwa.

##### **4.5.2 Kompyuta**

Kifaa hiki kimetumika katika kuchapa ripoti ya utafiti huu kama inavyoonekana. Kifaa hiki pia kimetumika katika kukusanyia data za upili pale mtafiti alipokuwa akisoma makala na vitabu mbalimbali katika wavuti na tovuti.

### **4.5.3 Hojaji**

Mtafiti aliandaa hojaji ambazo alizigawa kwa watafitiwa husika ili wajaze majibu kulingana na maswali waliyoulizwa. Hojaji hizi zilijazwa na baadaye kurudishwa kwa mtafiti tayari kwa kuchambuliwa.

### **4.5.4 Dodoso**

Mtafiti aliandaa dodoso ambalo alitumia kama muongozo wa kufanyia usaili na watafitiwa aliowateua. Dodoso hilo lilitumika na kusaidia kupatikana kwa data zilizohitajika.

## **4.6 Matatizo katika Ukusanyaji wa Data**

Hakuna tafiti inayokamilika katika sura maridhawa hasa kwa wanataaluma wa fani hiyo bila kupambana na matatizo ya aina yoyote. Katika kuiandaa na kuikamilisha pekuzi hii, yapo baadhi ya matatizo ambayo mtafiti alikumbana nayo katika ukusanyaji wa data. Miongoni mwa matatizo hayo ni suala la kutafautisha tanzu mbalimbali za semi, hasa tafauti ya methali na semi zilizoenea ambazo si methali mfano wa semi zilizoko hivi sasa katika lugha ya Kiswahili kama: imekula kwako ni msemu unaotumika kumaanisha kwamba mtu amekosa kitu alichokuwa anakitafuta, huu ni msemu ulionea sana kwa watumizi wa lugha ya Kiswahili hasa katika jiji la Dar es salaam, hata ukinawa huli, n.k.

Tatizo lingine kubwa alilokumbana nalo mtafiti ni lile la ugumu wa mawasiliano ya kilugha kati yake na jamii ya Kitanzania. Ugumu ambao amekwishaeleza kirefu katika Tatizo la utafiti.

#### **4.7 Data Zilizokusanywa**

Zaidi ya methali 110 zilikusanywa katika utafiti huu ambapo methali 80 zimefanyiwa uchambuzi wa kina (kwa kuonesha Tarjama zake) na maana yake kwa Kiswahili. Baadhi ya methali hizo, zimetumika katika utafiti huu kuthibitisha nafasi ya methali katika jamii ya Walibya na Watanzania. Methali zimewekwa kama Kiambatishi katika utafiti huu.

#### **4.8 Hitimishi**

Sura hii imefanya uwasilishaji wa mbinu mbalimbali za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya data za utafiti wetu. Mbinu hizi kama zinavyoonekana hapo juu zimetusaidia kwa kiwango kikubwa kupata data muafaka zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti wetu. Kutokana na ukweli huu tunaweza kuthibitisha kauli ya wanataalimu wa masuala ya Kiutafiti kwamba ili utafiti wowote ule wa kitaalimu ama kisayansi uweze kukamilika na kutoa matokeo stahiki ni lazima utafiti huo ufanywe kwa kuongozwa na mbinu sahihi za utafiti. Ripoti ya utafiti wetu inathibitisha jambo hili.

## **SURA YA TANO**

### **5.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI**

#### **5.1 Utangulizi**

Hii ni sura mama katika utafiti wetu. Ni sura mama kwa sababu ndiyo hasa inajibu maswali ya utafiti na kisha kutimiza lengo kuu la utafiti wetu. Kothari (2008) anaeleza kwamba utafiti wowote ule wa kitaalimu hauwezi kukamilika mpaka data zilizokusanywa ziwasilishwe, zichambuliwe na kujadiliwa. Sura hii inafanya kazi hii muhimu kama ifuatavyo:

#### **5.2 Uchambuzi wa Data**

Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kifasihi. Uchambuzi wa kifasihi ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo hutoa fursa kwa mtafiti kusoma, kutazama ama kusikiliza jambo la kifasihi kama vile wimbo, shairi, hadithi ama igizo na kisha kutoa maelezo juu ya dhamira na vipengele mbalimbali vya kisanaa vinavyounda jambo hilo la kisanaa (Kothari, 2008). Katika utafiti huu mtafiti alikusanya kwanza methali mbalimbali za Kiswahili na za Kilibya kisha akazipanga vizuri katika makundi kulingana na maudhui yake. Baada ya hapo alianza kuchambua data za utafiti wake kulingana na madhumuni mahususi ya utafiti wake. Uchambuzi huo ni kama unavyoonekana hapa chini.

#### **5.3 Kuainisha Methali Zinazofanana**

Imeeleweka kwamba Libya na Tanzania ni nchi za Afrika, ambazo licha ya kutofautiana kijiografia lakini bado zinafanana katika baadhi ya tamaduni zake,

hivyo basi kuwepo kwa mfanano wa methali si jambo la ajabu. Katika hilo mtafiti amechagua jumla ya methali 80 ambazo katika hizo methali 40 ni za Kilibya na 40 nyingine ni za Kiswahili. Ambazo zinahusu dhamira za elimu, udugu, malezi, kujali chako, maonyo na masuto.

### 5.3.1 Elimu

Mtafiti amependa kutanguliza methali za elimu, kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa elimu katika kuiendeleza jamii yoyote ile. Methali za elimu zitakazoandikwa hapa zitaweka wazi kazi kubwa ya fasihi simulizi ya methali katika kuchochea maendeleo, hivyo na kuthibitisha kuwa fasihi simulizi ni kiungo kisichokubali badala katika falsafa ya maisha ya binadamu. Kinyume na baadhi ya mitazamo ya Wanataaluma wa fasihi wanaodai kuwa fasihi simulizi haihesabiwi katika fasili za fasihi pale inapozungumziwa fasili ya fasihi.<sup>9</sup> Hebu tuone mfano wa methali za Kiswahili na zile za Kilibya zinazohusu elimu.

#### **Methali ya Kiswahili**

Kuuliza si ujinga

#### **Methali ya Kilibya**

النشدها دلاً لآداب

<sup>9</sup> Mwenda Ntaragwai 2004 akifasiri maneno ya Ndiposa anasema: (Ndiposa Okot P' Bitek (1973:18) anasema:

Katika usomi wa kimagharibi, fasihi humaanisha maandishi ya wakati au nchi fulani, hasa ile yenye kupewa thamani ya juu katika mtindo na uendelezaji wake. Ufafanuzi huu unaotilia mkazo uandishi walenga kueleza kwamba fasihi ni amali ya jamii zilizovumbua sanaa ya uandishi.- tafsiri yetu. )

Ntaragwai anaendelea kueleza: Kwa hivyo, fasihi, kulingana na mtizamo huo wa kimagharibi, imechukuana na uandishi, na hivyo basi fasihi si fasihi mpaka iandikwe. Bila shaka mtizamo kama huu hupuuza fasihi-simulizi. Ama kwa hakika hiyo hatua ya kuihusisha fasihi na maandishi ni ya maksuudi inayodhamiriwa kuonyesha fasihi kama amali ya jamii yenye taaluma ya kusoma na kuandika. Ni kile kitendo cha kibinafsi au cha kubagua ambacho hudhamiria kuonyesha jamii ambazo hazina taaluma ya uandishi kama jamii duni.



**Latini:** Annashad addall a dhahab

**Tarjama:** Kuuliza humuongoza mtembeaji

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi zimnahimiza mtu kuuliza jambo asilolijua

### **Methali ya Kiswahili**

Akuangushaye hukufunza kupigana.

### **Methali ya Kilibya**

الليعضك فكر كفياسنو ناك

**Latini:** Elle adhwak fakkarak fisnuunak

**Tarjama:** Aliyekung'ata amekukumbusha kutumia meno yako

**Matumizi:** Hizi ni methali zinazotufunza umuhimu wa kujifunza kutokana na makosa yetu.

### **Methali ya Kiswahili**

Asiyeuliza hana ajifunzalo

### **Methali ya Kilibya**

الليمايشاور مايدير أصحاب

**Latini:** Ellee ma yshaawir maa yidiir ashaab

**Tarjama:** Asiyetaka ushauri hana rafiki

**Dhima ya methali hizi:** Huwanasihi watu wasione haya au ubaya kuuliza kama wanataka kujifunza

### **Methali ya Kiswahili**

Msafiri huonja mapishi mengi

### **Methali ya Kilibya**

كل سفر هاتعلمك احداقه

**Latini:** Kullua safrah t-allaamak hdaagah

**Tarjama:** Kila safari hukufundisha jambo jipya.

**Dhima ya methali hizi:** Methalli hizi hutumiwa kufahamisha kwamba anayesafiri hupata matukio tofauti ambayo humfunza.

### **Methali ya Kiswahili**

Aulizaye si mjinga; mjinga ni asiyeuliza

### **Methali ya Kilibya**

قلوب الرجال مخازن

**Latini:** Guluubul rijaal makhaazin

**Tarjama:** Nyoyo za watu ni hazina

**Dhima ya methali hizi:** Hizi ni methali zinazotuhimiza tusione aibu kuuliza maswali ili tujifunze. Kuuliza juu ya jambo fulani ndiko kulifahamu vizuri jambo hili kwa kuwa majibu yatakayotolewa yatakuwa na maarifa pamoja na ujuzi ndani yake.

Si hivyo tu bali pia, zipo methali nyingine zinazohimiza umuhimu wa kutumia elimu na maarifa ya kitaalimu katika shughuli mbalimbali badala ya kutumia nguvu katika kufanya shughuli hizo. Mfano wa methali hizo katika jamii ya Waswahili na ile ya Walibya ni ifuatayo:

### **Methali ya Kiswahili**

Elimu haina mwisho

### **Methali ya Kilibya**

يموت المعلمو هو يتعلم

**Latini:** Yamuut lmuallim, wohuu yat allam

**Tarjama:** Mwalimu hufa ilhali bado anajifunza

**Dhima ya methali hizi:** hizi ni methali zinzomtaka mtu kutotosheka na elimu aliyokuwa nayo. Badala yake anatakiwa ajitahidi katika kutafuta elimu zaidi na zaidi mpaka afike katika ngazi za juu kielimu.

Vile vile, katika jamii ya Waswahili na ile ya Walibya kuna methali zinazohimiza kutembea sehemu mbalimbali duniani kwa ajili ya kutafuta elimu. Elimu haipatiakani mahali pamoja na kila mahali panaweza kuwa na maarifa tofauti na mahali pengine. Hivyo basi kutembelea mahali hapo kwa ajili ya kujifunza kutamfanya mtu apate maarifa mapya katika taalimu yake au yoyote ile. Hebu tuone mfano wa methali zifuatazo:

**Methali ya Kiswahili**

Elimu hushinda nguvu

**Methali ya Kilibya**

اللي عند عقل ما يعتاز لبدنقه

**Latini:** Ellee in-dah akl maa yaataaz libandagatah

**Tarjama:** Mwenye akili hahitajii bunduki

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi zinatuhimiza kutumia elimu katika mambo yetu na sio kutumia nguvu.

**Methali ya Kiswahili**

Ahangaikanye sana na jua hujua.

**Methali ya Kilibya**

الراجل صندوق مسكر مفتاحها التجارب

**Latini:** Al raajil sondoug msakkar, miftaahah al tajaarob

**Tarjama:** Binadamu ni sanduku lilofungwa, funguo yake ni kujaribujaribu

**Matumizi:** Methali hizi huwafunza watu umuhimu wa kutaalamika katika mambo ya ulimwengu. Ni vizuri kutembea na kujifunza mambo ya ulimwengu.

Katika jamii ya Waswahili na ile ya Walibya zinazo methali zinazoeleza umuhimu wa elimu katika jamii na kwamba elimu ni hazina kubwa katika maisha ya mwanadamu. Methali zifuatazo zinathibitisha hili.

### **Methali ya Kiswahili**

Elimu ni mali ambayo adui hawezi kuteka

### **Methali ya Kilibya**

ما حسدنا هم في المال، حسدونا في وسعة البال

**Latini:** Maa hasadnaahum fil maal, hasaduuna fii wos atil baal

**Tarjama:** Hatukuwahusudu katika mali zao, wametuhusudu kwa uelewa Wetu.

### **Methali ya Kiswahili**

Elimu nguvu ya mwanadamu

### **Methali ya Kilibya**

اللي اقر الصفتي ماير يد مفتي

**Latini:** Ellee graa al switfiy maa yriid muftiy

**Tarjama:** Aliyesoma vizuri hahitajii mufti

**Dhima ya Methali:** Hutumiwa kutushauri umuhimu wa kuwa na elimu ambayo ni hazina tusiyoweza kunyang'anywa na adui yeyote.

Kwa upande mwingine tunakutana na methali zinazohimiza umuhimu wa mtu kuwa na elimu katika maisha yake. Methali hizo ni:

### **Methali ya Kiswahili**

Elimu ni mwangaza

### **Methali ya Kilibya**

القاريا علخير

**Latini:** Algaariy alaa kheyr

**Tarjama:** Msomi yupo kwenye kheri

**Dhima ya methali hizi:** Hutukumbusha manufaa yanayotokana na elimu. Elimu ndiyo mwangaza wa maisha ya mwanadamu katika shughuli zake za kila siku. Iwapo mwanaadamu atakosa elimu basi ni dhahiri kwamba, maisha yake yatakuwa magumu sana.

Si hivyo tu bali pia, elimu humsaidia mwanadamu kutatua migogoro baina yao kwa njia ya amani badala ya kutumia silaha hatarishi kwa maisha yao. Kwa mfano methali zifuatazo zinaeleza kwamba:

### **Methali ya Kiswahili**

Kalamu hushinda upanga

### **Methali ya Kilibya**

الليكتب غلب

**Latini:** Ellee katab ghalab

**Tarjama:** Aliyeandika ameshinda

**Dhima ya methali hizi:** Hizi ni methali zinazotukumbusha uwezo mkubwa wa elimu au maarifa yanayotokana na maandishi, yanaweza kuwa na uwezo mkubwa wa kubadili jamii kuliko kutumia upanga au nguvu.

Pia, kupitia methali za Kiswahili na Kilibya tunaelezwa kwamba elimu haina mwisho. Mifano ya methali zifuatazo zinathibitisha hoja hii.

### **Methali ya Kiswahili**

Elimu ni bahari haishi kwa kuchotwa

### **Methali ya Kilibya**

العلم بحر

**Latini:** Al ilm bahar

**Tarjama:** Elimu ni bahari

**Dhima ya Methali hizi:** Methali hizi zinatumiwa kwa ajili ya kutukumbusha kuwa elimu haina mwisho, na madamu binadamu bado anaishi hakosi jambo jipya la kujifunza.

Baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusu kufafana kwa methali za Kiswahili na zile za Kilibya katika masuala ya elimu ni vema sasa tutazame kufanana kwa methali hizo katika kipengele cha udugu.

## **5.4 Udugu**

Kusudio la mtafiti katika anuani hii (udugu) linalenga ndugu, rafiki, jirani au jamaa wa karibu mwenye nafasi kama ya ndugu. Wahenga na wahenguzi walijua umuhimu wa udugu katika maisha ya binadamu, hivyo hawakuona kwamba ni busara kuviacha vizazi vinavyokuja pasi na kuvikumbusha jambo hili muhimu. Na ndipo walipotoa methali zinazomhamasisha mtu kushikamana na aliyekaribu yake na kumsamehe endapo atakosea. Jamii mbili za Kitanzania na Kilibya zimetekeleza dhima hii kwa kiasi kikubwa, na zifuatazo ni baadhi tu ya methali zilizozungumzwa katika dhamira hii. Mfano wa methali zinazozungumzia suala la udugu ni hizi zifuatazo:

**Methali ya Kiswahili**

Isipowasha hunyeza

**Methali ya Kilibya**

الدمايخناؤلو فلْمُوَزَّرَه

**Latini:** Addam yhinn oulao fil muwazzara.

**Tarjama:** Damu husikitisha hata kama ni Machinjioni

**Dhima ya methali hizi:** zinamaanisha kwamba damu ya mtu wa karibu hata kama haikuwasha kwa uchungu wa udugu basi itanyeza. Methali nyingine ni:

**Methali ya Kiswahili**

Damu ni nzito kuliko maji

**Methali ya Kilibya**

الدممايرقدش

**Latini:** Addam maa yergudish

**Tarjama:** Damu hailali

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi hutumiwa sana wakati mtu fulani anapomtetea au anapomsaidia jamaa yake dhidi ya asiyekua jamaa yake, hata ikiwa jamaa yake ndiye mkosa.

Katika jamii ya Waswahili na ile ya Walibya zipo methali zenye kuonya juu ya wanajamii kugombana kwa sababu wagombanaji hupata hasara badala ya faida katika tendo hilo. Kwa mfano, methali zifuatazo zinaeleza kuwa:

**Methali ya Kiswahili**

Vita ya panzi neema ya kunguru

### **Methali ya Kilibya**

اتعاركو الخواتم حوال المهبولات

**Latini:** At aarakou lakhawaat farhuu lmahboulaat

**Tarjama:** Kugombana kwa ndugu furaha kwa wajinga

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi hutumiwa kuonyesha kwamba wawili wanapogombana (au makundi mawili) anayepata faida ni mtu wa tatu. Wao hupata hasara tu. Kwa hiyo wajitahidi wasigombane.

Umoja na mshikamano ni jambo muhimu katika maendeleo ya jamii yoyote ile hapa duniani. Jamii ya Waswahili na ile ya Walibya zina methali zinazoeleza umuhimu wa umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii kama ifuatavyo:

### **Methali ya Kiswahili**

Kidole kimoja hakivunji chawa.

### **Methali ya Kilibya**

العينة تقتل الصيد

**Latini:** Al-eena tagtul al sweid

**Tarjama:** Kushirikiana huua kiwindwa

**Dhima ya Methali hizi:** Methali hizi hutumiwa kuhimiza watu washirikiane katika mambo yao.

Suala la kuvumiliana miongoni mwa wanajamii nalo limezungumzwa katika jamii zote mbili yaani ile ya Walibya na Waswahili. Udugu wa kweli utapatikana pale tu wanandugu watakapovumiliana kutokana na mapungufu yao kama binadamu. Methali zifuatazo zinashadadia hoja hii.



**Methali ya Kiswahili**

Kuishi na ndugu ni kuvumiliana

**Methali ya Kilibya**

الليداير هالذيماكار ههالكأب

**Latini:** ellee daairah dheeb maa karhah lakalab

**Tarjama:** Analolifanya mbwa mwitu, mbwa halichukii

**Methali ya Kiswahili**

Kosa moja haliachi mke

**Methali ya Kilibya**

اسواد العظممايقلعها المصخون

**Latini:** Aswaad al adham maa yeglaahul maskhoun

**Tarjama:** Weusi uliopo kwenye mfupa hauondolewi kwa maji ya moto

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi hutumiwa kumfunzamtu kuwa na subirana ustahamilivu, asiwe na hasira za kuachana na jamaa yake wa karibu au rafiki yake. Baada ya kuzungumza kwa kina juu ya methali zinazozungumzia udugu sasa tugeukie zile zinazozungumzia malezi katika jamii.

**5.5 Malezi**

Lengo kuu la methali ni kumnyoosha mtoto, kumpa busara mtu mzima na kumuelimisha mjinga n.k. Kwa kuwa huwezi kumpa busara mtu mzima ambaye hakupata malezi bora hapo utotoni mwake, wala kumuelimisha mjinga ambaye hakuanza kufunzwa na wazazi au walezi wake, inadhihiri faida ya malezi katika kipindi cha utotoni ili kumuandaa binadamu mwenye kujitambua na kutilia

umuhimu busara, hekima na elimu. Na kwa ajili ya hili mtunzi ameona kuna ulazima wa kukusanya methali linganishi zenye dhamira ya malezi.

Ikumbukwe kwamba hakuna kizazi bora kitakachojenga mustakbali na maendeleo mazuri ya maisha kama kizazi kilichostaarabika kwa elimu, lakini kizazi hicho huwa ni vigumu kukipata kama hakijaandaliwa kwa malezi yaliyo bora mazuri sana, kwani elimu bila adabu ni sawa na utuuzima bila hekima, na kusoma ni kustaarabika. Kwa umuhimu huu wahenga na wahenguzi waliona ni jambo lililo zuri watuachie methali za malezi ili kuukamilisha uutu wa binadamu. Methali za malezi za Kilibya na Kitanzania zifuatazo zinaweka wazi jambo hili. Methali hizo ni kama zifuatazo:

#### **Methali ya Kiswahili**

Ukicha mwana kulia utalia wewe

#### **Methali ya Kilibya**

بكيك قبلما يتيك

**Latini:** Bakki eelak gabal maa ybakkiik

**Tarjama:** Mlilie mwanao kabla hajakuliza

#### **Methali ya Kiswahili**

Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

#### **Methali ya Kilibya**

ارباية البنت علي أمها

**Latini:** Rbaayat albint alaa umhaa

**Tarjama:** Malezi ya binti ni jukumu la mama

**Matumizi:** Methali hizi hutumiwa kuhimiza wazazi wawalee watoto wao vizuri ili wainukie na adabu nzuri.

**Methali ya Kiswahili**

asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

**Methali ya Kilibya**

الليمار بهاشبو هلياً ماير بوه

**Latini :** Ellee ma rabahhash buuh layyaam yrabbuuh

**Tarjama:** Asiyefunzwa na babaye, siku zitamfunza

**Matumizi:** Methali hizi hutumiwa kuwakumbusha wazazi na jamaa zake mtoto kuwa ni wajibu wao kumfunza mtoto wao.

**Methali ya Kiswahili**

Mti huchongewa ni (na) tundaze

**Methali ya Kilibya**

اللياضنباتشافي

**Latini:** Ellee dhnee baat shaagiy

**Tarjama:** Aliyezaa hubeba kesi za Wanawe.

**Matumizi:** Methali hizi hutumiwa kuonyesha kuwa mzazi huchongewa na wanawe, wanawe wakiwa hawana adabu watu watakuwa waki walaumu au wakiwatukana wazazi wao.

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi hutumiwa kumfunza mtu hatari au hasara ya kutomkanya mwanawe. Iwapo mzazi hatomfunza mwanawe nidhamu basi mtoto huyo atakuwa na nidhamu mbaya ambayo itamfanya afundishwe na ulimwengu. Wakati mwingine mtoto kama huyu humtendea ubaya mzazi wake kwa kuwa

hakumfunza tabia nzuri alipokuwa mdogo. Hivyo basi wazazi wote wanaaswa kuhakikisha kwamba wanawafunza watoto wao nidhamu nzuri wawapo watoto ili wasije wakaacha kufunzika wawapo watu wazima na kulazimika kuuachia ulimwengu uwafunze. Baada ya kuona methali zinazozungumzia suala la malezi sasa tutazame kipengele cha kuthamini kilicho chako.

### **5.6 Kuthamini Kilicho Chako**

Kibaya chako si kizuri cha mwenzo. Siku zote mwenye akili huwa anathamini kitu chake, pasi na kuangalia kitu hicho kina uzuri au thamani ya kiasi gani. Hii ni kwa sababu kitu cha kuazima huwa hakina muamana wa kwamba kitatosheleza malengo yanayokusudiwa katika muda muwafaka kabla ya kutakiwa na mwenye mali yake. Kwa kuzingatia hili wahenga wameona kwamba ni muhimu wawahimiza watu juu ya umuhimu wa mtu kujali kitu chake na kuangalia vipi akitunze, na si kutamani, kutegemea au kujali kitu cha mtu mwingine ambacho pengine hakitomtoshela. Methali zifuatazo zineelezea dhamira hii:

#### **Methali ya Kiswahili**

Nguo ya kuazima haisitiri matako

#### **Methali ya Kilibya**

العريّة ماتكسي

**Latini:** Al ariyyah maa taksiy

**Tarjama:** Nguo ya kuazima haisitiri

#### **Methali ya Kiswahili**

Mtumai cha ndugu hufa yu (hali) masikini

### **Methali ya Kilibya**

يا عابيا علمر قهجير انهايطو لاليلأو تأكلها بحساه

**Latini:** Yaa aabiy alaa marga jiiraanah, ituul leel ou laa taakul bihsaah

**Tarjama:** Mtumai mchuzi wa jirani, usiku utaingia na ataishia kulamba tu.

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi hutumiwa kumfunza mtu ajitegemee yeye mwenyewe asitegemee cha mtu mwingine, maana kinachomsitiri mtu ni kile chake, cha watu hakiwezi kumsitiri.

Vile vile, katika jamii zote mbili yaani ile ya Waswahili na Walibya zote zinatumizi ya methali zinazoelezea umuhimu wa kuthamini na kushughulikia jambo ama shughuli uliyonayo kwa wakati huo kuliko kufikiria jambo usilokuwa nalo. Mfano wa methali zifuatazo unashadadia hoja hii.

### **Methali ya Kiswahili**

Moja shika si kumi nenda rudi

### **Methali ya Kilibya**

عصفور في اليد أو لا منعشر هفشجر

**Latini:** Usfuur filyad oulaa min ashra f shajar

**Tarjama:** Bora ndege mmoja mkononi kuliko kumi mtini

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi hutumiwa kuonyesha kuwa ni bora kushika au kushughulika na ulichonacho kuliko kutumaini ambacho hujapata.

Vile vile, tunafahamishwa kwamba, katika jamii ya Waswahili na ile ya Walibya zipo methali ambazo zinazungumzia umuhimu wa kutosheka na kidogo ulichonacho kuliko kutamani kikubwa cha mwezako. Mfano wa methali zifuatazo ufafanua zaidi juu ya hoja hii.

**Methali ya Kiswahili**

Cha kupewa hakishibishi

**Methali ya Kilibya**

الضايقة ماتشبع

**Latini:** Aldhaaiga maa tshabbaa

**Tarjama:** Cha kuonja hakishibishi

**Methali ya Kiswahili**

Fumo lililo mkononi ndilo fumo.

Fumo ni mkuki

**Methali ya Kilibya**

أيهنخير.. العصافيدكو الافيد غير

**Latini:** Ayyuhunna kheir. Al asaa fiidak wallaa fiid gheirak

**Tarjama:** Ni kipi bora. kuwa na fimbo mkononi mwako au kuwa na fimbo mkononi mwa mwenzako.

**Methali ya Kiswahili**

Kimfaacho mtu chake

**Methali ya Kilibya**

ماينفعك الا خمستك الليفيدك

**Latini:** Maa yanfaak illaa khamsatak f iidak

**Tarjama:** Hakitakufaa isipokuwa ulichoshika mkononi mwako

**Methali ya Kiswahili**

Kibaya chako tunza cha mwenzio sio chako.

**Methali ya Kilibya**

الليماير قعايده، مايلقنجديد الناس

**Latini:** Ellee ma yiraggaa baaydah maa yalgaa jadiid al naas

**Tarjama:** Asiyeziba kiraka cha nguo yake chakavu, hapati nguo mpya za watu

**Methali ya Kiswahili**

Jinga ni lako mwenyewe, la mwenzio huwezi kuitumia

**Methali ya Kilibya**

اضرب بمنقار كما ينفع

**Latini:** Udhrub bimun gaarak maa yanfaa zey

**Tarjama:** toboa kwa tindo yako, ya kuazima haitafaa

**Methali ya Kiswahili**

Fimbo ya jirani haiwezi kuua nyoka

**Methali ya Kilibya**

اللي يتكلع ليزاد غير هيطول جو عهليله

**Latini:** Ellee yattakil alaa zaad gheirah yetuul juu leylah

**Tarjama:** Mtegemea chakula cha mtu, huumwa njaa usiku kutwa

**Methali ya Kiswahili**

Kanzu ya kuazima usiendee Ijumaa

**Methali ya Kilibya**

الثوب العريّة ما يدقّي

**Latini:** Althoub al ariiyyah maa ydaffiy

**Tarjama:** Nguo ya kuazima haizuii baridi

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi zinatufunza umuhimu wa kutosheka na vitu vyetu hata kama sio vizuri. Kitu chako si sawa na cha kupewa. Pia methali hizi zinakumbusha kwamba kitu kitakachokufaa katika dhiki na hata faraja ni kile ulichonacho kwa wakati ule na sio kitu kilichopo mikononi mwa mwenzako. Methali

hizi pia zinaendelea kukumbusha kwamba, usitegemee kitu cha mwenzako katika kutatua shida zako bali pambana na jitahidi kutafuta cha kwako ili ukitumie kutatua shida zako.

### **5.7 Tahadhari (Maonyo na Masuto)**

Siku zote huwa ni vizuri mtu akachukua tahadhari katika mabo yake ili asiye kujuta baada ya kufanya jambo ambalo hakuwa makini nalo. Wahenga waliona umuhimu wa jambo hili wakaamua kutuachia methali kadhaa ambazo zinaakisi umuhimu wa tahadhari katika maisha ya binadamu. Methali zifuatazo zinaonesha umuhimu huu:

#### **Methali ya Kiswahili**

Hadhari kabla ya hatari

#### **Methali ya Kilibya**

ابعد علشر أو غنيله

**Latini:** Ab ad al sharr oughanniyy lah

**Tarjama:** Epuka shari na iimbe

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi zinatufunza umuhimu wa kuwa na hadhari kabla ya kutenda mambo. Kutenda jambo bila ya kutafakari kwa kina kunaweza kuleta madhara makubwa katika jamii ama kwa mtu binafsi. Hivyo basi kupitia methali hizi wanajamii wa Wakitanzania na wale wa Libya wanaonywa kwamba, wasipende kutenda mambo mbalimbali bila kufikiria vya kutosha.

Vile vile, katika jamii hizi mbili zipo methali zinazoeleza umuhimu wa kuchukua tahadhari juu ya watu ambao ni wakorofi na wapenda shari. Miongoni mwa methali hizo ni:



**Methali ya Kiswahili**

Akumulikaye mchana usiku atakuchoma.

**Methali ya Kilibya**

الليامدور كلاقك

**Latini:** Ellee mdawrak laagiik

**Tarjama:** Anayekutafuta kwa ubaya atakupata

**Methali ya Kiswahili**

Aliye kando haangukiwi na mti

**Methali ya Kilibya**

تَبْعَاطِرَافَلَانْدَعَدَعَلَاتَخَاف

**Latini:** Tabbaa latraaf laa tadda daa laa tkhaaf

**Tarjama:** Tembea pembeni mwa njia hutadhuriwa wala kumuudhi mtu.

**Methali ya Kiswahili**

Dulu liumalo silipe kidole

**Methali ya Kilibya**

مُتَوْرِيْعَشْكَالطَيُورَلْيَخْرَبُوْه

**Latini:** Matwarrii ash shak lityourliikharbuuh

**Tarjama:** Usiwaoneshee ndege kiota chako, watakiharibu.

**Methali ya Kiswahili**

Fimbo impigayo mke mwenzio ukiiona itupe nje

**Methali ya Kilibya**

اللياتعشخو كاتغداك

**Latini:** Ellee t ashaa khuuk et ghaddaak

**Tarjama:** Aliyemfanyia uadui nduguyo atamalizia kwako.

### **Methali ya Kiswahili**

Alalaye usimwamshe ukimwamsha uta lala wewe.

### **Methali ya Kilibya**

عمرَ كَمَا تَقُولُ لِلْعَرِيَانِ وَيَنْثُوبَكَ

**Latini:** Umrak maa t-goul lil aryaan wein Thoubak?

**Tarjama:** Usithubutu kumwambia aliye uchi iko wapi nguo yako?

**Matumizi:** Ni methali zinazotututahadharisha kwamba tusije kujiingiza katika matatizo yasiyotuhusu tukapata majuto baadae.

### **Methali ya Kiswahili**

Oto la kuku usililaze kichwechwe

### **Methali ya Kilibya**

عمرَ كَمَا تَحْطَرُوسَ الْكِلَابِ عَالِوَسَايِدَ

**Latini:** Umrak maa t-hut rousul kilaab al- wasaaaid

**Tarjama:** Usithubutu kuweka kichwa cha paka kwenye mto.

**Matumizi:** Ni methali ambazo zinatutahadharisha kumpatia mtu mwenye shida ya kitu fulani, kumpatia kitu hicho hicho akutunzie, atakitumia tu.

**Dhima ya methali hizi:** Methali hizi zinatufundisha tutahadhari na watu waovu ambao waliwahi kutufanyia ubaya au fititna tukanusurika, kwa kuwa wametukosa kwa hili watatafuta jingine la kutuamamiza. Pia methali hizi zinakumbusha kwamba ni vema mtu akimbaini mwenye shari basi akae pembeni yaani aachane naye na asijibishane naye. Si hivyo tu, bali pia mtu akimjua mtu fulani kwamba ni muovu basi asizoeane naye. Vile vile, kupitia baadhi ya methali hizi tunafahamishwa kuchukua tahadhari juu ya mabaya yaliyomfika mwezetu ili yasije yakatufika sisi

pia. Methali hizi pia zinamuonya mwanadamu asithubutu kujiingiza katika mambo yasiyomuhusu kwa kuwa yatamletea matatizo. Vile vile, mwanadamu huyu anaonywa asiye akampatia mtu mwenye shida kitu fulani amuhifadhi kitu ambacho huyo mwenye shida ndiyo anashida ya kitu kama hichohicho. Akiamua kumpatia mtu huyo kitu hicho basi aelewe kwamba kitu hicho kitatumiwa.

### **5.8 Mfanano Uliopo kati ya Methali za Kilibya na Kitanzania Kimaudhui na**

#### **Fani**

Ni vema kwanza tukafahamu ni nini maana ya maudhui na nini maana ya fani kabla ya kuona maudhui au fani hiyo inafanana vipi kati ya methali za jamii mbili hizi. Tafiti zilizokusanywa katika kitabu kiitwacho: Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili (Chuo Kikuu cha Dar es salaam) inaeleza kwamba: Maudhui ni mambo makuu yanayojadiliwa katika fasihi. Ni mawazo ambayo ndiyo yaliyomchochea mwandishi asilia kuamua kuandika riwaya au tamthilia au ushairi. Naye Masebo na Nywangwine kwa upande wao wameielezea maudhui kuwa ni mambo yaliyomo (yanayozungumza) ndani ya shairi. Maudhui katika kazi ya fasihi ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumlisha mawazo, pamoja na mafunzo yaliyomsukuma msanii hadi kutunga kazi fulani ya fasihi.

Ama fani hii ni zile (njia anazozitumia mtunzi kuyasawirisha maudhui yake kwa hadhira yake). Masebo na Nyangwine. Maudhui na fani ni ala ambazo zinashirikiana kujenga kitu kimoja, ila ushirikiano huu umeleta tofauti kati ya wanalughawiya, wapo ambao wameuona ni kama ushirikiano uliopo kati ya mtu na nduguye na wapo waliouona ni kama mtu mmoja ambaye hakamiliki ila kwa

viungo vingine vya mwili. Hitilafu hii imepelekea kutokea kwa istilahi mbili za mitazamo ya uhusiano huu. Mtazamo wa kwanza ni mtazamo wa Kidhanifu, na wa pili ni wa Kiyakinifu.

Ama mtazamo wa kwanza huu unawahusha kina Profesa Sengo, Kiango na wengine wanaoona kuwa, fani na maudhui ni vipengele ambavyo havina uhusiano wowote, na kwamba kila kimoja kinajitegemea. Ni kwamba vinaweza kutenganishwa. Ama mtazamo wa pili ambao ni wa Kiyakinifu huu unawakilishwa na kina Senkoro, Mulokozi na wengineo, ambao wanaona kuwa fani na maudhui ni vitu visivyoweza kutenganishwa, na huathiriana na kutegemeana. Maudhui ni mawazo yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa msanii juu ya mawazo hayo, fani ni ule ufundi wa kisanaa anaotumia msanii kuwasilisha mawazo hayo kwa jamii inayohusika. (Nadharia ya Fasihi ya Kiswahi juzuu 2).

Senkoro anasema (Fasihi 2011) Baadhi ya wananadharia wamehusisha mahusiano hayo na yale ya sehemu ya ndani ya chungwa ambayo inaliwa (maudhui) na sehemu ya ganda la chungwa ambayo kwa kawaida hutupwa (fani). Udhaifu mkubwa wa Istilahi na nadharia hizo ni kuwa, zinatenganisha vitu ambavyo kimsingi havitenganishwi, *fani na maudhui ni sura au pande mbili za sarafu moja*; na si rahisi wala sahihi kuzitenga na kuzieleza katika upweke... *kwani fani imo ndani ya maudhuina maudhui nayo yamo ndani ya fani*.

Pamoja na hitilafu za wanataaluma hao juu ya mtazamo wao katika mahusiano ya fani na maudhui lakini bado inaonyesha kuwa hivyo ni vitu viwili ambavyo

hakuna budi kimoja kuwa na mwenziwe. Katika methali za Kilibya na Kitanzania kuna mfanano mkubwa wa kimaudhui, kwani zote zinazungumzia elimu, udugu, malezi, kujali chako pamoja na maonyo na masuto. Pia methali za jamii hizo zinafanana katika baadhi ya fani zake ambazo baadhi yake ni kama zifuatazo:

### 5.8.1 Msisitizo Bayana

Msisitizo bayana ni kusisitiza maana ya sentensi kwa kutumia kinyume chake (Masebo na Nyambari). Tamathali hii hutumika pale wakati mtu huwa anataka kumfafanulia msomaji au msikilizaji kwamba ukitaka kujua ubaya au uzuri wa jambo hili hebu angalia upande mwingine ili iwe wazi kwako. Katika methali za Kilibya zilizotumia tamthali hii ni kama zifuatazo:

#### 1- Kwa Kilibya:

الليمار بهاشبو هليامايروه

#### Kwa Kilatini:

Ellee ma rabbahaash buuh layyaam yrabbuuh

#### Tarjama

Asiyefunzwa na babaye, siku zitamfunza.

#### 2- Kwa Kilibya:

عصفور فياليدأوللمنعشرة فشجر

#### Kwa Kilatini:

Usfuur filyad oulaa min ashra f shajar

#### Tarjama:

Bora ndege mmoja mkononi kuliko kumi mtini

#### Kwa Kilibya

الليماير قعايد همايا قجديد الناس

**Kwa Kilatini:**

Ellee ma yaraggaa baaydah ma yalgaa jadiid al naas

**Tarjama:** Asiyeziba kiraka cha nguo yake chakavu, hapati mpya za Watu.

**Kwa Kilibya:**

4 بكعياك قبلما يبكياك

**Kwa Kilatini**

Bakki eelak gabal maa ybakkiik

**Tarjama:**

Milie mwanao kabla hajakuliza

**Kwa kilibya**

5 اضر بيمنقار كما ينفعز يو

**Kwa Kilatini**

Udhrub bi min gaarak maa yanfaa zeyyu

**Tarjama**

Toboa kwa tindo yako, yakuazima haitafaa

Methali za Kiswahili zenye msisitizo bayana ni kama zifuatazo:

- 1 Aulizaye si mjinga; mjinga ni asiyeuliza
- 2 Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu
- 3 Ukicha mwana kulia, utalia wewe
- 4 Moja shika, si kumi nenda uje
- 5 Kibaya chako tunza, cha mwenzio sio chako

6       Jinga ni lako mwenyewe, la mwenzio huwezi kutumia

7       Alalaye usimwamshe, ukimwamsha utalala wewe

### 5.8.2 Takriri Dufu

Takriri maana yake ni kujirudia. Goldsmith ((Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili - Chuo Kikuu cha Dar es slaam)) aneleza kuwa Takriri ni kujirudia koktekwa sauti au silabu katika maneno mawili au zaidi ya mstari ambayo huleta umuhimu fulani wa kisanaa, kama vile kusesitiza, sauti ya kuvutia au hata sauti isiyovutia. Nyanwine na Masebo wao wanaielezea takriri kuwa ni urudiaji wa herufi, silabi, maneno au sauti zinazolingana katika kazi ya sanaa.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo ina ujazo mkubwa wa takriri katika sentensi au silabi zake. Carolyn A. Parker (Semina ya Kimataifa) anafafanua sababu ya wingi huu kuwa: Lugha ya Kiswahili ni rahisi sana kuwa na Takriri kwa sababu ya silabi zake za wazi na vokali zake zenye hali maalum ya kifonolojia, mambo ambayo bila shaka husaidia katika kusababisha wingi wa aina aina hii ya Takriri katika methali.

Takriri ina vigawanyo zaidi ya viwili kati ya hivyo ni kile kinachojulikana kama Takriri dufu. Hii ni ile aina ya kukaririka kwa irabu mbili au zaidi katika kila neno ndani ya kifungu kimoja cha sentensi, ni mara chache hupatikana katika konsonanti, mfano:

Aibu ya maiti aijuaye ni mwosha.

Na zifuatazo ni methali za Kilibya zenya Takriri dufu

### Kwa Kilibya

- 1 اللّيمائشاور مايدير أصحاب

#### Kwa Kilatini

Ellee maa yshaawir maa ydiir as-haab

**Tarjama:** Asiyetaka ushauri hana rafiki

### Kwa Kilibya

- 2 اللّيمائير قعايد همايلقنجديد الناس

#### Kwa Kilatini

Ellee maa yargaa baaydah maa yalgaa jadiid alnaas

#### Tarjama

Asiyeziba kiraka cha nguo yake chakavu, hapati mpya za watu.

- 3 تبعطرافلاتد عد علا تخاف

Tabbaa latraaf laa taddai laa tkhaaf

**Tarjama:** Tembea pambozoni mwa njia hutadhuria wala hutamuudhi mtu.

Methali za Kiswahili zenye Takriri Dufu ni kama Zifuatazo:

- 1 Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
- 2 Hadhari kabla ya hatari
- 3 Fimbo impigayo mke mwenzio ukiiona itupe nje

### 5.8.3 Vina

Abdul kaahir Al jurjaaniy (Jawaahirul balaaghah 2004) anaeleza kuwa vina ni kufanana kwa herufi ya mwisho katika sentensi mbili. Masebo na Nyangwine wanaeleza kwamba vina ni silabi za namna moja zinazotokea baada ya kila



mizani kadhaa katika mstari wa shairi. Ujumla wa maelezo yaliyotangulia hapo juu unaonesha kuwa vina ni mfanano wa herufi ya mwisho katika jumla ya sentensi, sawa sawa iwe shairi, nathiri au jumla yoyote ya maneno inayokusanya sentensi kuazia mbili na zaidi.

Methali kwa kuwa zina fungu A na B inamaanisha zinabeba zaidi ya kifungu kimoja cha maneno, hapa kuna umuhimu wa kuvichunguza vifungu hivyo katika upande wa vina. Si kwamba methali ili iwe ni methalil yenye ujumbe mzito inatakiwa iwe na urari wa vina, la hasha! Isipokuwa vina vina mchango fulani katika kunasisha ujumbe uliokusudiwa kwa msikilizaji au msomaji hasa wale wenye uonjo wa kisanaa. Methali za Kilibya zifuatazo ni baadhi ya methali zenye vina katika lugha hiyo:

### **Kwa Kilibya:**

1 الليعضك فكر كفياسنونك

### **Kwa Kilatini**

Ellee adhwak fakkarak fisnuunak

### **Tarjama**

Aliyekung'ata amekukumbusha kutumia meno yako

2 الليداير هالذييماكار ههالكليب

### **Kwa Kilatini**

Ellee daairah dheeb maa karhah lakalab

### **Tarjama**

Analolifanya mbwa mwitu , mbwa halichukii

3      بكعيلك قبلما يكيك

**Kwa Kilatini**

Bakki eelak gabal maa ybakkiik

**Tarjama**

Mlilie mwanao kabla hajakuliza

4      الليتشخوكتغداك

**Kwa Kilatini**

Ellee t ashaa khuuk etghaddaak

**Tarjama**

Alimfanyia ubaya nduguyo nawe atakufanyia

Methali za Kiswahili zenye vina ni kama zifuatazo

1      ahangaikaye sana na jua hujua

2      mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

3      tahadhari kabla ya hatari

#### **5.8.4 Muundo wa Methali**

Methali za Kilibya na za Kiswahili zinafanana kimuundo, ni kwamba zote zina muundo wa lugha ya mkato fupi na yenye kueleweka haraka kwa msikilizaji au momaji.

#### **5.9 Tafauti Iliyopo kati ya Methali za Kilibya na Kitanzania Kimaudhui na**

##### **Kifani**

Ingawaje methali za Kilibya na za Kiswahili zinazfanana katika maudhui na baadhi ya tanzu za fani, ila kuna tofauti zinazopatikana katika methali hizo. Miongoni mwa tofauuti hizo ni:

- 1 Kifani, wakati methali za Kiswahili zinaweza kuwa na mtindo wa kishairi wenye mizani kati ya mitano mpaka kumi takriban, kama tunavyosoma katika haba na haba hujaza kibaba 5/6 na mtaka cha mvunguni sharti ainame 8/7.

Methali za Kilibya zenya mtindo wa kishairi haziko hivyo , mtindo wa kishairi katika methali za Kilibya huchukua zaidi ya mizani hiyo. Mfano ni kama methali ya Kilibya ifuatayo:

لونهر فكيادار يماكشدار يلا نعر كلا اندير فيكضرا ري

**Kilatini:** Lau naarfak yaa daari, maa kash daari ,

Laa na amrak lan diir fiik edhraariy

**Tarjama:** Lau ningejua kama kwamba hii nyumba yangu kuwa sio ya milele, nisngejenga wa kuzaa.

- 2 Kimazingira, wakati vijana wengi wa Kilibya wanazifahamu sana methali za “ Kujali chako” kuliko nyenginezo kama tulivyogundua hili katika hojaji mbalimbali tulizowafanyia, tunakuta vijana wa Kitanzania wanazifahamu sana methali za “ Udungu” kuliko nyenginezo.

- 3 Chuku nyingi zinazotumika katika methali za Kilibya huashiria hali ya hewa mgawanyiko ya nchi hiyo, kama vile ile methali inayosema: (Nguo ya kuazima haizuii baridi) na nyenginezo ambazo zinaashiria uwepo wa kipindi cha baridi kali katika nchi hiyo.

Methali nyingi za Kiswahili hutaja mimea au miti ambayo inaakisi mazingira halisi ya Tanzania kwamba ni ardhi ya rotuba inayokubali mazao.

## **5.10 Sababu za Kufanana na Kutafautiana kwa methali za Kilibya na Kiswahili**

### **5.10.1 Sababu za Kufanana Kifani**

Mtafiti anaona kuwa kuna sababu nyingi zilichangiakutafautianakwamethali za Kilibya na Kitanzania katika fani, lakini wenda ikawa sababu kuu za zilizoleta mfanano huo ni mbili ambazo kama anavyoona mtafiti, ambazo ni:

#### **A. Umoja Wa Bara**

Libya na Tanzania licha ya kutafautiana Kijiografia ila bado zitabaki kuwa ni nchi zilizomo ndani ya bara la Afrika. Uwepo huu unafaradhisha kufanana kwa baadhi ya tamaduni, ada na tabia ambazo huzaa methali.

#### **B. Misafara ya Kibiashara**

Inafahamika kwamba tangu hapo zamani na mpaka hii leo nchi nyingi zimekuwa na mabadilishano ya kibiashara. Maingiliano haya kati ya mataifa mbalimbali yalisababisha kuhamisha hata baadhi ya tamaduni kutoka katika nchi moja kupeleka nchi nyingine. Nchi za Afrika zilikuwa pia na mabadilishano haya, Libya na Tanzania zikiwemo.

### **5.10.2 Sababu za Kutafautiana Kifani**

#### **A. Lugha**

Kila lugha ina kanuni, masharti na sifa ambazo huzitafautisha na lugha nyingine. Kwa mfano wakati lugha ya Kiswahili inaruhusu kuanza na konsonati ambazo zinaweza kutumika katika neno bila msaada wa irabu, kwa zile konsonanti zenye silabi kubwa kiasi cha kuziwezesha kutamkika, mfano: mke, nchi na nyinginezo,

katika lahaja ya Kilibya ni lazima kuanza kwa konsonanti yenye irabu. Hivyo basi hata katika mtindo wa shairi la Kilibya kuna masharti yake ambayo yanatafautiana na masharti ya shairi la Kiswahili. Na hii ndiyo siri ya kutofautiana baadhi ya ani za fasihi za jamii mbili hizi.

### **B. Mazingira**

Kwa upande wa mazingira sababu zilizowafanya vijana wa Kilibya kujali methali nyingi za” kujali chako” kuliko nyinginezo ni ile siasa ya ujamaa waliyodumu nayo kwa zaidi ya miongo mine. Ama kwa vijana wa Tanzania kufahamu methali nyingi za “ Udugu” kuliko nyinginezo ni kwa sababu ya hali ya amani wanayodumu nayo kwa takriban miongo mitano tangu kupatikana kwa uhuru wa nchi zao.

### **5.11Hitimishi**

Sura hii imefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti kwa mujibu wa madhumuni mahususi ya utafiti huu. Kwa ujumla sura hii inaonesha kwamba kuna mfanano mkubwa wa kimaudhui na kifani kati ya methali za Kiswahili na zile za Kilibya. Ufanano huu unathibitisha nadharia za Kifasihi kwamba fasihi katika sehemu mbalimbali duniani imejengwa kwa vipengele vinavyofanana na kwamba dhima kuu ya fasihi ni ile ile katika sehemu mbalimbali duniani. Vile vile, tumebaini tofauti kadhaa baina ya methali za Kiswahili na zile za Kilibya. Sura inayofuata inawasilisha muhtasari, hitimishi na mapendekezo.

## **SURA YA SITA**

### **6.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **6.1 Utangulizi**

Sura hii ndiyo ya mwisho katika utafiti huu ambayo hutoa muhtasari na mahitimisho ya jumla ya utafiti mzima pamoja na kutoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye. Tumeanza sura hii kwa kutoa muhtasari na hitimishi kisha kufuatiwa na mapendekezo.

#### **6.2 Muhtasari na Hitimishi**

Utafiti huu umejenga na sura kuu nne ambapo ndani yake kuna mada ndogo ndogo zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti wetu. Sura ya kwanza imewasilisha vipengele muhimu vya utangulizi wa utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, lengo la utafiti, madhumini mahususi na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafiti pamoja na utatuzi wake na mwisho ni mipaka ya utafiti.

Sura ya pili ya utafiti huu imefanya mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti ili kusaidia kubainisha tatizo la utafiti. Mapitio ya maandiko yamesaidia katika kuonesha kwamba hakuna utafiti wa kina uliokwisha fanyika mpaka sasa katika kulinganisha na kutofautisha methali za Kiswahili na za Libya kwa katika vipengele vya fani na maudhui. Hivyo basi utafiti huu umefanywa ili kuweza kuziba pengo hili la kiutafiti kama lilivyobainishwa kwa kutokuwepo marejeleo juu ya kufanana na kutofautiana kwa methali za jamii ya Kiswahili na Kilibya. Sura iliyofuata imewasilisha nadharia za utafiti.

Sura ya tatu ya tasnifu hii imewasilisha juu ya nadharia mbalimbali za fasihi ambazo zimetumika katika kuuongoza uhakiki wa methali za Kiswahili na Kilibya kama inavyoonekana katika sura ya nne ya tasnifu hii. Miongoni mwa nadharia zilizowasilishwa ni ile ya Simiotiki, Umarx na kadhalika. Nadharia zote hizi zimetusaidia kuhakiki methali zinazohusu masuala mbalimbali katika jamii ya Waswahili na kulinganisha na kutofautisha na zile za Walibya. Sura iliyofuata imefanya uwasilishaji wa mbinu mbalimbali za utafiti.

Sura ya nne ya utafiti huu imefanya uwasilishaji wa mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti. Miongoni mwa mbinu hizo ni pamoja na usanifu wa utafiti, ukusanyaji wa data za msingi na zile za upili. Data za upili zimekusanywa kupitia mbinu ya kusoma machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti katika maktaba zilizoteuliwa. Data za msingi zimekusanywa kupitia mbimu za usaiji, hojaji na ushuhudiaji. Vile vile, vipengele vya sampuli na usampulishaji navyo vimewasilishwa. Sura inayofuata imewasilisha na kuchambua data za utafiti.

Sura ya tano ya utafiti huu imefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa minajili ya kujibu maswali ya utafiti wetu. Pamoja na mambo mengine sura hii imeonesha kwamba, upo mfanano mkubwa katika methali za Kiswahili na zile za Kilibya katika dhamira za elimu, malezi, udugu, maonyo na marudi, kuthamini ulichonacho nakalika. Vile vile, katika fani imebainika kwamba kuna uhusiano mkubwa katika vipengele vya lugha, takiriri na masuala ya msisitizo. Sura ya mwisho katika utafiti huu ilihusu kutoa muhtasari, hitimishi na mapendekezo.

### 6.3 Hitimishi

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, methali za Kiswahili na zile za Kilibya zinaufanano mkubwa katika dhima ya methali hizo kwa jamii husika. Nyingi kati ya methali hizi zinaonesha kwamba dhima kubwa ya methali katika jamii kuadilisha na kuonya wanajamii juu ya mambo mbalimbali ambayo yanaonekana kuwa si mazuri na yana madhara kwa wanajamii wote. Katika utafiti huu tumebaini kwamba, methali za Kiswahili na zile za Kilibya zinawaonya wanajamii kutokuwa wategemezi kwa mali za ndugu zao na badala yake wafanye kazi kwa bidii ili kila mtu aweze kumiliki mali yake kwa kuwa mtegemea cha ndugu hufa masikini.

Vile vile, katika methali hizi tumebaini kwamba katika jamii zote mbili zipo methali zinazohimiza umuhimu wa wazazi kuwapatia watoto wao malezi bora ili wawe na tabia nzuri zinazokubaliwa na wanajamii wote. Iwapo itatokea mzazi hakumfunza mwanawe basi ulimwengu utamfunza tena kwa mikikimikiki ambayo inaweza kuhatarisha maisha na usalama wake. Tunasema hivi kwa sababu kama motto akiwa mdokozi wa mali za watu basi anaweza kuadhibiwa na wanajamii wenye hasira kali mpaka akafariki dunia. Hivyo basi, kila mzazi amfunze mwanae kabla ulimwengu haujamfunza.

Pia, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba katika jamii zote mbili kuna methali zinazohimiza kila mwanajamii kuhakikisha kwamba anatafuta elimu kwa njia yoyote ile ili aweze kuwa na maarifa ya kuendeshea maisha yake. Elimu ndio ufunguo wa maisha ya mwanaadamu popote pale alipo hivyo ni wajibu wa kila mwanajamii kulichangamkia suala hili bila kusukumwa au kulazimishwa na mtu fulani katika kusoma. Utafiti huu pia umetuonyesha kwamba jamii mbili za Libya na Tanzania zinashirikiana katika baadhi ya



tamaduni zake, na zote licha ya kuwepo kwa tofauti za kijiografia, siasa na vyanzo vya uchumi, zinafanana katika baadhi ya mambo ya fasihi.

Utafiti pia umeweza kutuonyesha kuwa kuna uhusiano usiovunjika kati ya jamii mbili hizi unaodumishwa na kazi za fasihi. Hii ni kusema kwamba ijapokuwa siasa na sera za nchi mbili zinatofautiana, jambo ambalo linaifanya nchi moja kuingalia nchi nyingine kama mpinzani wake kimitazamo ya kisiasa ila fasihi iliyomo ndani ya jamii hizi inawafanya wajione kuwa ni ndugu wa asili.

Matokeo ya utafiti pia yameonesha kwamba, methali za Kiswahili na zile za Kilibya zinafanana katika vipengele vya matumizi ya lugha, vina na takriri. Kwa upande wa Lugha kuna matumizi ya lugha ya picha, ishara, taswira na sitiari.

#### **6.4 Mapendekezo**

Kwanza kabisa, Kwa kuzingatia kuwa waarabu walifika pwani ya Afrika Mashariki tokea karne ya 8, na walipofika wenyeji wa eneo hilo walikuwa wakizungumza lugha zao za kibantu Kiswahili kikiwa ni moja ya lugha hizo. Na kwamba waarabu hao walilazimika kujifunza Kiswahili ili wapate kufanikisha malengo yao ya kidini, biashara na ya kijamii. Kutokana na hayo mtafiti anaona kuna umuhimu wa kuandika methali linganishi kati ya Kiswahili na lugha ya *Kiarabu Fasaha* ili kuona ni taathira gani ya kitamaduni iliyojificha katika mahusiano hayo ya zamani.

Pili, mtafiti anaona kwamba kuna ulazima mkubwa wa kufasiri vitabu vya fasihi ya Kiswahili kuviingiza katika Kiarabu na vya Kiarabu kuviingiza katika Kiswahili. Hili ni kwa lengo la kuwapa wepesi wale wapenzi wa fasihi wanaotaka kuchungulia fasihi za

wenzao. Hivyo anaziomba idara husika hasa wizara za elimu za nchi mbili hizi kulishughulikia hili ili kuendeleza mahusiano ya karbu kati ya fasihi ya Kitanzania na Nchi za Kiarabu.

## MAREJELEO

- Babbie, E., (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth.
- Bathes, R., (1994). *The Semiotic Challenge* Berkely: University of California Press.
- Balisidya, M. L. (1982), "Uchaguzi katika Fasihi Simulizi", *Mulika* namba 19, *cha Lugha* Juzuu no.2 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Chandler, D., (1992). *Semiotics: The Basics* London: Routledge Press.
- Cohen, L. na Wenzake, (2000), *Research Methods in Education* (5<sup>th</sup> Edition): London.
- Cooper, P. (1989), *Teaching Basic Gymnastics*, Macmillan Publishing: *Dar es Salaam*.
- Finnegan, R. (1970), *Oral Literature in Afrika*. London: Oxford University Press.
- Haraamah, A. (2002), *Warakaat fil- bahthi wal Kitaaba*, Imenezwa na Islamic call.
- Kaahir, A. (2005), *Jawaahirul balaaghah* - Chapa ya pili Al jurjaaniy: Maktabatul adaab.
- Kahigi, K. K. (1995), "Lugha katika vitabu vya Watoto", *Kioo Cha Lugha*, Juzuu, Na.1, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, kur.21-36.
- Khatibu, M. S. (1981), "Taarab ni Fasihi Simulizi?" Makala ya Semina, TUKI: Dar Kiangi S.D. na Sengo, T.S.Y. (1972), "Fasihi", *Mulika* Namba. 4, Dar Salaam: TUKI.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- King'ei, K. (1996), "Nafasi ya Nyimbo za Kiswahili za Taarab katika Jamii ya Kisasa". *Kioo Cha Lugha*, TUKI: Dar es Salaam.
- King'ei, K. (2011), *Kamusi ya Methali za Kiswahili*, East African Education: Nairobi.
- Kombo, D. Ketel, (2006), *Production and Thesis Writing: Introduction*, Nairobi.

- Kothari, R.C. (2008), *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: New Age Publishers Limited.
- Lakoff, G. na Wenzake, (1980), *Metaphor We Live By*, Chicago:University of London: Rutledge Falmer Press.
- Longhom (2001), *Kamusi ya Karne ya 21: Kamusiya Kiswahili*, Nairobi: Longhom Publishers.
- Maryam Abdulhamid (2002), *Methali za Kiswahili Maana na Matumizi Juzuu 1-3* Kimeenezwa maktabat bin hamoudah, Chapa ya kwanza.
- Masebo na Nyangwine, N.C.M (2009), *Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili kidato cha 5&6*, Nyambari Nyangwine Pulishers: Dar es Salaam.
- Masebo, J.A na Nyangwine, N.C.M. (2007), *Nadahria ya Fasihi Kidato cha 5 na 6* Nyambari Nyangwine Publishers: Dar es Salaam.
- Masebo, J.A, na Nyangwine, N.C.M. (2009), *Nadharia ya lugha ya Kiswahili cha Kidato cha 1-4* Dar es Salam; Nyambari Nyangwine Publishers.
- Mhilu G. (2008), *Tahakiki ya Vitabu Teule 3 na 4 Nadharia Uhakiki na Maswali*, Dar es Salaam: Mkuki na nyota publishers: Dar es Salaam.
- Mlacha, S. A. K. (1981), *Methali Kama Chombo Muhimu katika Jamii. Makala za TUKI*: Dar es Salaam.
- Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi fupi*, Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Mtesigwa, P. C. K. (1989), *Methali ni nini?* Mulika Juzuu na 55, TUKI: Dar es Salaam.
- Mulokozi M. M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili Dar es Salaam*, TUKI: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

- Mulokozi, M. M. (1989), *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Mulika namba 21 TUKI: Dar es Salaam.
- Munshid, M., (2004), *Allugha Walkitaabal Liibiyah Kadiimah*, Chapa ya Kwanza.
- Mustafa, A. (2002), *Al- taabiir al Shaabiyah Al liibiyahAl-misraatiy*, Chapa ya Pili.
- Mturo, N. (2011), “Matumizi ya Lugha katika Semi ziandikwazo katika Daladala Jijini Dar es Salaam”, Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.
- Ndungo, C. W. (1991), *Misingi na Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*, Nairobi: University of Nairobi.
- Ndungo, C. W. (1993), *Nadharia ya Fasihi simulizi*, Nairobi: University of Nairobi.
- Njogu, K. na Rocha. C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi, JKF.
- Nsookwa, J. (2011), “Dokezo za sitiari katika methali za Kiswahili na Kiganda”, Chuo kikuu cha Makerere: Kampala.
- Ntaragwi, M. (2004), *Uhakiki wa kazi za fasihi*, Augustana College: Rock Island.
- Ramadhan, A. (2012), *Nadhras shariyah ilaa taabiir Shaabiyah Liibiyah Ganoud*. Omar Mukhtaar- Libya.
- Robson, C., (2007). *How to do a Reserch Project: A Guide for Undergraduate Students*, Carton Victoria: Blackwell Publishing.
- Sengo, T. S. Y. (1979), *Fasihi Smulizi: Urithi wa Utamaduni wetu*, Dar es Salaam: AKADEMIYA.
- Sengo, T. S. Y. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi*, Dar es Salaam: AERA.
- Senkoro, F.M.E.K., (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.
- Senkoro, F.E.M.K., (2006). “Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi simulizi na Fasihi andishi”, katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili chuo kikuu cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Senkoro, F.E.M.K. (2011), *Fasihi*, Kautu Limited: Dar es Salaam.

Wamitila, K.W., (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi:  
Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*,  
Nairobi: Vide-Muwa.

Wamitila, K.W. (2011), *Lulu za lugha, Kamusi ya Methali*, Longhorn publishers:  
Nairobi.

Wizara ya Elimu na Utamaduni, (2003), *Monduli ya Somo la Kiswahili, Somo la 1*,  
Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Yin, R.K., (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2<sup>nd</sup> eds. Thousands  
Oaks Calif: SAGE publishers

Zeid Abdu (2006), *Vitendawili na ukuaji wa lugha nchini Libya na Tanzania*,

## VIAMBATISHO

### **Kiambatisho Namba 1: Dodoso kwa Ajili ya Usaili, Walengwa ni Wazee**

#### **Utangulizi**

Mimi ninaitwa Hamza ni mwanafuzi wa shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninafanya utafiti huu ili kukamilisha masharti ya kumaliza shahada yangu. Naomba nikuulize maswali machache ili nipate data ya kukamilisha utafiti huu.

#### **Taarifa za Utambulisho**

Jina..... Umri.....  
 Kiwango cha Elimu..... Kuoa/kuolewa.....

#### **Maswali**

1. Naomba unitajie methali zisizopungua ishirini unazozifahamu.
2. Taja dhamira inayowasilishwa kupitia kila methali uliyoitaja.
3. Eleza mazingira zinamotumika methali mbalimbali ulizoitaja.

**Asante kwa ushirikiano wako**

This image shows a full page of white paper with ten horizontal dashed lines, typical of primary school handwriting practice paper. The lines are evenly spaced and extend across the entire width of the page. There is no text or other markings on the paper.



2. Taja dhamira inayowasilishwa kupitia kila methali uliyoitaja.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. Eleza mazingira zinamotumika methali mbalimbali ulizozitaja.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

**Asante kwa ushirikiano wako**